Nipashe
Alhamisi Juni 11, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580255
www.ippmedia.com
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Watoto wawili walivyouawa kwa kucharangwa mapanga

UKURASA 8




UKURASA 11

# Maalim Seif aibua mambo 10 Uchaguzi Mkuu Oktoba

**AZITAKA** NEC, ZEC kutenda haki, pia uchaguzi utakaoacha furaha kwa Watanzania...*Endelea ukurasa 2*




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mkutano wa kuwakaribisha wanahisa wa Benki ya CRDB wakati wa Mkutano Mkuu wa 25, utakaofanyika kupitia mtandao mwezi Juni 27, mwaka huu. Kulia ni Ofisa Mkuu wa Fedha wa benki hiyo, Fredrick Nshekanabo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## BAA LA CORONA



Shirika la Afya Duniani (WHO), linashauri kuwa kwenye eneo ambalo kuna mkusanyiko mkubwa wa watu unaofanya kushindwa kukaa kwa umbali ulioshauriwa, serikali ihamasishe uvaaji barakoa za kushona ambazo zimezingatia ubora.

* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**



## SHAMBULIO LA MBOWE LAVIIBUA VYAMA

UKURASA 2

# Macho, masikio bungeni bajeti mwaka 2020/21 leo

UKURASA 3




**MICHEZO** YANGA, MOLINGA KIMENUKA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Viongozi upinzani walaani Mbowe kushambuliwa

**Elizabeth Zaya na Mary Geofrey**

VIONGOZI wa vyama vitatu vya siasa nchini wamelaani tukio la kushambuliwa kwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe na watu wasiojulikana.

Viongozi hao ni Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Self Sharif Hamad, Makamu Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu na Mwenyekiti wa TLP, Augustino Mrema.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Maalim Seif alisema kitendo hicho si cha kiungwana na kinapaswa kulaaniwa na kila mtu.

Aliwakemea baadhi ya watu wanaokejeli kitendo cha kuumizwa Mbowe ambaye pia ni Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni (KUB) ambacho alikiita si cha kiungwana.

"Watanzania tulikotoka huko nyuma, tusingeweza kufikiria kwamba kitendo kama hicho kingetokea, najiuliza kwamba Tanzania tumepoteza utu kiasi gani, mwenzako amefikwa na maafa halafu wengine wanamkejeli," alisema.

Naye, Makamu Mwenyekiti wa Chadema, Lissu alizitaka taasisi za dini, za kijamii, kiraia na watetezi wa haki za binadamu kulaani tukio hilo na kulipinga kwa kuwa halina sura ya utu.

Lissu amedai hakuna matumaini wala matarajio yoyote ya uchunguzi utakaofanywa na Jeshi la Polisi nchini, na kwamba ni wajibu wao (wadau, taasisi na watu) kuendelea kulisemea na kukemea uhalifu kama huo wenye mlengo wa kuua demokrasia.

"Kitendo kilichofanyika cha kumshambulia mbunge na KUB ni cha kigaidi. Mashambulizi haya ya kisiasa yanafanywa kwa lengo la kisiasa bila kuzingatia limefanywa na serikali, taasisi zake au mtu binafsi ni ugaidi," alisisitiza Lissu.

Alisema Chadema na taasisi zenye nia njema na taifa, zinawajibu wa kutoendelea kukaa kimya kuhusu tukio hilo ambalo alidai ni mwendelezo wa matukio mengi ya aina hiyo.

Vile vile, alidai Mbowe alishambuliwa kama alivyoshambuliwa yeye mwaka 2017 wakati akirejea nyumbani kwake jijini Dodoma, lakini hadi leo hakuna aliyewahi kukamatwa wala kuchukuliwa hatua kuhusiana na tukio hilo.

"Hatuna haja ya kusubiri uchunguzi wa Jeshi la Polisi kwa sababu hawatafanya kitu chochote licha ya kuwa tukio hili ni la kigaidi," alidai Lissu.

Kadhalika, alisema, hoja iliyotolewa na Spika wa Bunge, Job Ndugai, bungeni juzi akidai kuwa Mbowe alikuwa amelewa, Lissu alisema kwa mujibu wa sheria za Tanzania kulewa siyo kosa.

Kwa mujibu wa Lissu, hakukuwa na tamko la katazo la hali ya hatari nchini ambayo ingewalazimu watu kuchukua tahadhari.

Naye, Mwenyekiti wa TLP, Mrema alisema amepokea kwa masikitiko taarifa za kuvamiwa na kuumizwa kwa Mwenyekiti Chadema.

Mrema ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Parole, alivitaka vyombo vya dola kuharakisha uchunguzi na kuwachukilia hatua wale wote waliohusika na tukio hilo.

Mbowe alishambuliwa na watu wasiojulikana kwa kukanyagwakanyagwa maeneo ya tumboni na kujeruhiwa eneo la mguu wa kulia, na kwa sasa anaendelea na matibabu Hospitali ya Aga Khan, jijini Dar es Salaam.



Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, akizungumza na waandishi jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Zanzibar, Haji Duni Haji. **PICHA: JUMANNE JUMA**.

# Maalim Seif aibua mambo 10 Uchaguzi Mkuu Oktoba

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, ametaja mambo kumi ya kuzingatia ili Uchaguzi Mkuu Oktoba, mwaka huu uwe huru na haki.

Aidha, amezitaka Tume ya Uchaguzi Tanzania (NEC) na Tume ya Taifa Zanzibar (ZEC), kuhakikisha zinatenda haki kuliko kugeuka kuonea vyama vya upinzani.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Maalim Seif, alisema ni vyema uchaguzi ukawaacha Watanzania wakiwa na furaha na matumaini kwa kutekeleza wajibu wao wa kidemokrasia wa kuchagua viongozi wanaowataka.

"Kwa bahati mbaya mazingira ya kisiasa nchini kwa sasa hayatoi taswira ya uchaguzi unaoweza kuiacha nchi salama. Tunakwenda kwenye uchaguzi huku taifa likiwa halina umoja na likikosa maelewano ambayo yangefanikisha uchaguzi kufanyika kwa amani," alisema Maalim Seif, ambaye aliwahi kugombea urais wa Zanzibar katika uchaguzi wa mwaka 1995, 2000, 2005, 2020 na 2015 na kushindwa, huku akidai kushinda na kuilaumu ZEC kutomtangaza kuwa mshindi.

"Tunakwenda kwenye uchaguzi Taifa likiwa katika mazingira mabaya na mfumo mbovu wa uendeshaji chaguzi kuliko wakati mwingine wowote wa historia yetu."

Aidha, alisema ni vyema vyombo vya dola vikahakikisha haviendeshwi kwa muundo wa kuonea au kuumiza wengine bali kwa namna itakayolivusha taifa salama kwenye "Dalili zipo wazi kuwa kama hali ya sasa itabaki kama ilivyo, bila shaka uwezekano wa amani tunayojivunia huenda ikawa ni historia. Tunawasihi wenye mamlaka wasiifikishe nchi huko," alisema Maalim Seif.

Maalim Seif aliziomba NEC na ZEC kuhakikisha zinafanyia kazi mapendekezo yao kumi, ambayo wanaamini kwamba ni kikwazo katika uchaguzi mkuu ujao ili kuhakikisha yanaboreshwa na uchaguzi unakuwa huru na haki.

**Mambo 10**

Maalim Seif alitaja mambo kumi kuwa ni kuhakikisha zinapatikana tume huru za uchaguzi katika pande zote mbili za Muungano.

Pili, aliitaka serikali kutathmini makosa yaliyofanyika katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika Novemba mwaka jana na ipeleke muswada kwa hati ya dharura bungeni na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ili kufanya mabadiliko ya Katiba na sheria za Uchaguzi.

Tatu, aliitaka ZEC kumaliza kuondoa hujuma zinazofanywa katika kazi ya uandikishwaji wa wapigakura Zanzibar na kuhakikisha kila mwananchi mwenye sifa anaandikishwa na kupata kitambulisho cha mkaazi.

Nne, alisema hawakubaliani na kitendo cha ZEC kupunguza idadi ya majimbo.

"ZEC imetangaza dhamira yake ya kutaka kupitia upya idadi na mipaka ya majimbo ya uchaguzi Zanzibar. Ni jambo la kushangaza kwa sababu mwaka 2015 iliongeza majimbo kutoka 50 hadi 54. Si jambo lililotarajiwa hata kidogo kuona kuwa ZEC watafikiria kukata majimbo baada ya miaka mitano tu tokea kukata majimbo hayo," alisema Seif.

"Taarifa za uhakika za ndani ya ZEC tulizonazo zinaonyesha mipango ya ZEC inalenga kupunguza majimbo kutoka 54 waliyoyaongeza mwaka 2015 na kurudi kuwa 50, lakini katika muundo tofauti na uliokuwapo kabla ya mwaka 2015," alisema na kuendelea:

"Katika kufanikisha hili, wanalenga kupunguza majimbo mawili kisiwani Pemba na majimbo mengine mawili katika wilaya za Magharibi Unguja."

Sita, alizitaka NEC na ZEC zishirikishe wadau vya kutosha katika utungaji wa kanuni za uchaguzi na ushiriki wa waangalizi wa kimataifa na wawakala wa vyama vya upinzani na kutaka ziweke pia sharti kwa vyama vya upinzani kupewa nakala za daftari la wapigakura mapema kabla ya kampeni kuanza.

Saba, alizitaka mahakama zijirekebishe na kurudisha imani ya wananchi katika kusimamia na kutoa haki na kuwataka Majaji na Mahakimu pamoja na Maofisa wengine wa mahakama kutenda haki.

Nane, Jeshi la Polisi kuhakikisha linalinda usalama wa raia na mali zao kwa kutenda haki katika kipindi cha uchaguzi mkuu.

Tisa, aliwataka wakuu wa mikoa, wilaya, wakurugenzi wa Halmashauri pamoja na vyombo vya habari vya umma kutotumika vibaya au kuegemea kwa chama chochote cha siasa katika uchaguzi mkuu ujao.

Kumi, alisema ACT-Wazalendo kitahakikisha kwamba chaguo la wananchi wa Zanzibar linaheshimiwa.

"Tutahakikisha tunaungana na wananchi kuona mshindi wa uchaguzi wa mwaka 2020 anapata fursa ya kuunda serikali bila mizengwe na hila kama ambavyo Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 inavyotaka," alisema Maalim Seif.

"Huu utakuwa ni uchaguzi wa sita tokea kuanzishwa kw a mfumo wa vyama vingi, wananchi wa Zanzibar wameshuhudia kila aina ya hila zikifanyika kuzuia chaguo lao kupata nafasi ya kuongoza nchi,"alisema.

"Yaliyofanyika yanatosha. Tunataka watawala wajue kuwa jaribio lolote la kuwanyima tena wananchi wa Zanzibar fursa ya kuongozwa na kiongozi wanayemtaka hatutolikubali, ACT Wazalendo itasimama na umma wa Wazanzibari kuzuia jaribio hilo, watawala wajiandae kuwajibika na matokeo ya jaribio hilo, nilisema mwaka jana narudia tena kuwa sasa basi imetosha."

HABARI KITAIFA



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Taifa, Rais Dk. John Pombe Magufuli, akiendesha Kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya chama hicho, Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**.

# Macho, masikio bungeni

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MACHO na masikio yanatarajiwa kuelekezwa bungeni jijini Dodoma leo wakati serikali itakapowasilisha makadirio ya bajeti yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Mpango wa Maendeleo ya Taifa na ukomo wa bajeti ya mwaka 2020/21, unaonyesha bajeti hiyo inatarajiwa kuwa ya Sh. trilioni 34.88, huku Sh. trilioni 21.98 zikitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikiwamo gharama za uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Bajeti hiyo ya mwisho kwa awamu ya kwanza ya serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli, imeongezeka kutoka Sh. trilioni 33.1 zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha (2019/20), sababu kuu ikitajwa kuwa gharama za uchaguzi mkuu.

Mbali na uchaguzi mkuu, bajeti hiyo pia imezingatia mahitaji halisi ya ugharamiaji miradi mikubwa ya kimkakati, ulipaji mishahara, deni la serikali na vipaumbele vingine vya taifa.

**MAPATO, MATUMIZI**

Kwa mujibu wa mpango huo uliowasilishwa bungeni Machi 11, mwaka huu, kiasi cha Sh. trilioni 34.88 kinachotarajiwa kukusanywa, kinajumuisha mapato ya ndani ya Sh. trilioni 24.07 (asilimia 69 ya bajeti yote), mikopo ya ndani Sh. trilioni 4.9, mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara Sh. trilioni 3.04 na misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo Sh. trilioni 2.87 (asilimia 8.2 ya bajeti yote).

Kwa mujibu wa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, kati ya fedha hizo, Sh. trilioni 21.98 zitakuwa za matumizi ya kawaida na Sh. trilioni 12.9 za matumizi ya maendeleo (asilimia 37 ya bajeti yote).

Bajeti ya maendeleo inajumuisha Sh. trilioni 10.16 ambazo ni fedha za ndani (asilimia 78.8 ya bajeti ya maendeleo) na Sh. trilioni 2.74 fedha za nje.

Pia Sh. bilioni 400 zitatumika kulipa madeni yaliyohakikiwa, ujenzi wa reli ya kati ya kisasa (SGR) Sh. trilioni 2.1, mradi wa umeme wa Julius Nyerere Sh. trilioni 1.6 na mingine ni Sh. trilioni 6.06.

**KICHEKO, KILIO**

Katika bajeti hiyo, kunatarajiwa kuwa na ongezeko na punguzo la tozo, ada na ushuru katika bidhaa mbalimbali zinazozalishwa ndani na nje ya nchi kama ilivyokuwa katika bajeti zilizopita.

Bidhaa zinazotarajiwa kuguswa ni pamoja na vinywaji baridi (soda, maji na juisi), sigara, mvinyo, pombe na pombe kali.

Maeneo mengine muhimu yanayotarajiwa kuguswa ni unafuu wa kodi kwenye sekta ya viwanda, kilimo, mifugo, madini na huduma muhimu za kijamii kwa lengo la kudhibiti mfumuko wa bei na kulinda viwanda vya ndani.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, aliweka wazi kuwa bajeti ijayo ya serikali itakuwa na punguzo la tozo, ada, kodi na ushuru kwenye sekta anazozisimamia (mifugo na uvuvi).

Serikali pia inatarajiwa kuondoa migongano ya sheria, kanuni na taratibu zinazotumiwa na mamlaka mbalimbali katika utozaji kodi na gharama kubwa za kuanzisha na kuendesha biashara kutokana na wingi wa kodi, ada na tozo zinazoambatana na taratibu zenye urasimu.

Vilevile, Sera ya Bajeti inabainisha kuwa kwa mwaka ujao wa fedha, serikali inatarajiwa kuwa na bajeti yenye mikakati ya kuondoa mianya na mazingira ya rushwa na mwingiliano wa majukumu na wingi wa mamlaka za udhibiti katika kuidhinisha na kutoa hati, vibali na vyeti kwenye shughuli za uwekezaji na biashara.

**VIPAUMBELE VINNE**

Kwa mujibu wa Waziri Mpango, bajeti ijayo itazingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17-2020/21.

Vipaumbele hivyo ni pamoja na viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda, serikali ikitarajia kujenga viwanda vinavyotumia kwa wingi malighafi zinazopatikana nchini zikiwamo za kilimo, madini na gesi asilia, ili kukuza mnyororo wa thamani.

Miradi hiyo ni pamoja na Ujenzi wa Kiwanda cha Kuchakata Gesi Asilia, uanzishwaji na uendelezaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi na Kongane za Viwanda, viwanda vya kuongeza thamani mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, kuongeza thamani ya madini na usimamizi endelevu wa rasilimali za misitu.

Pia, kuweka mkazo kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora, pembejeo na zana za kilimo na uvuvi, huduma za ugani na utafiti, uimarishaji wa malambo na majosho, ujenzi wa maghala na upatikanaji wa masoko ya mazao na mifugo ndani na nje ya nchi.

Kipaumbele kingine ni kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, serikali ikilenga kuboresha upatikanaji wa huduma za afya, elimu na ujuzi na huduma za maji safi na salama.

Shughuli za miradi zitakazotekelezwa ni pamoja na kugharamia utoaji wa elimumsingi bila ada, utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, kuboresha huduma ya maji, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni, kuimarisha elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, ununuzi na usambazaji wa dawa, ujenzi wa hospitali za wilaya na vituo vya afya.

Vilevile, kupunguza vifo vya kinamama vinavyotokana na uzazi, kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji nchini, kuimarisha huduma za ubora wa maabara za maji, kuboresha huduma za maji mijini na vijijini na kuimarisha usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Kipaumbele cha tatu ni uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji, miradi itakayotekelezwa ikilenga kuendelea ujenzi na ukarabati wa miundombinu nishati, usafirishaji na ununuzi na ukarabati wa ndege, meli na vivuko pamoja na uanzishwaji wa Kanda Maalumu za Kiuchumi.

Miradi hiyo ni pamoja na wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115; Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania; Ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kisasa (SGR) na kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini.

Kipaumbele cha nne ni kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa mpango wa serikali, serikali ikitarajia kuendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa na kuimarisha utawala bora katika usimamizi wa miradi ya maendeleo.

## Korti EACJ yatupa rufani ya serikali

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MAHAKAMA ya Afrika Mashariki (EACJ), imetupilia mbali notisi ya kukata rufani iliyopelekwa mahakamani na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya maombi yaliyofunguliwa na Baraza la Habari (MCT), Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) na Kituo cha Sheria cha Haki za Binadamu (LHRC).

Uamuzi wa kutoa ushindi kwa MCT na washirika wake umesomwa na Jaji wa Mahakama hiyo, Geofrey Kiriabwire, akiongozwa na majaji watatu akiwamo Jaji Sauda Mjasiri pamoja na Rais wa Mahakama hiyo, Emmanuel Ugirashebuja.

Upande wa MCT na washirika wake waliwakilishwa na mawakili watatu wakiongozwa na Fulgance Masawe, huku upande wa serikali ukiwakilishwa na Wakili Stanley Kalokola.

Awali, waleta maombi hao walipeleka maombi mahakamani hapo wakiitaka mahakama hiyo, itupilie mbali notisi ya kukata rufani iliyopelekwa mahakamani na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MCT, THRDC, na LHRC walipeleka maombi hayo ya kupinga vifungu kadhaa vya Sheria ya Huduma za Habari ya 2016 vinavyokinzana na vifungu vya mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Machi 28, 20120, maombi hayo, yalisikilizwa kwa mara ya kwanza Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki (EACJ) na Mahakama hiyo iliwapa ushindi MCT, THRDC na LHRC.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali alipeleka notisi ya rufani kwenye kitengo cha rufani cha Mahakama hiyo, Aprili 11, 2020, ili kupinga uamuzi huo.

Hata hivyo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilishindwa kuchukua hatua ya kupeleka maombi ya rufani ndani ya muda husika wa siku 30.

Kulingana na kanuni ya 86 ya Kanuni za Mwenendo wa Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki (EACJ) za 2013, Mwanasheria Mkuu alipaswa kupeleka maombi yake ya rufani ndani ya siku 30 tokea siku alipopeleka notisi hiyo ya kuonyesha nia ya kukata rufani.

Julai 9, 2020, Kitengo cha Rufani cha Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki, kilitoa uamuzi na kuamuru kuwa notisi ya kukata rufani ya Mwanasheria Mkuu imetupiliwa mbali kwa kushindwa kuchukua hatua za lazima katika kukata rufani hiyo.

HABARI KITAIFA

## Kiwanda Tanchoice kuanza kuchakata nyama mwezi huu

**Na Mwandishi Wetu**

KIWANDA cha kisasa cha nyama cha Tanchoice kilichopo Soga, wilayani Kibaha, mkoa wa Pwani, kinatarajia kuanza uzalishaji mwezi huu (Juni) ili kutumia fursa kubwa ya uhitaji wa nyama nchi za Asia unaotokana na kuibuka na kusambaa kwa ugonjwa wa corona duniani.

Kufuatia kuibuka kwa ugonjwa wa corona duniani, shughuli nyingi za kiuchumi zilisimama zikiwamo uchakataji wa nyama na kufanya uhitaji mkubwa wa bidhaa hiyo.

Mradi huo ambao uwekezaji wake ni zaidi ya Sh. bilioni 35 ni moja ya mafanikio makubwa ya miradi ya viwanda vilivyoanzishwa katika maeneo maalum ya uwekezaji baada ya kupata leseni kutoka Mamlaka ya Ukanda Maalumu wa Uwekezaji (EPZA).

Mkurugenzi wa EPZA, James Maziku, alisema kiwanda hicho kilitakiwa kuanza uzalishaji baadaye mwaka huu, lakini kutokana na uhitaji mkubwa wa nyama katika nchi za Asia ambako ndio soko lililokuwa limelengwa, kitaanza uzalishaji mwezi huu ili kutimiza hitaji hilo.

"Kiwanda hiki chenye kutumia tekinolojia ya kisasa kitakuwa na uwezo wa kuchakata ng'ombe 1,000 na mbuzi na kondoo 4,500 kwa siku, tayari kimezingatia viwango vya kitaifa na kimataifa ambavyo husimamiwa na Shirika la Viwanga Nchini (TBS) ikiwa ni pamoja na mfumo wa usimamiaji wa usalama wa chakula ISO 22000 na usimamizi wa mfumo wa ubora ISO 9001," alisema Maziku.

Kiwango cha nyama kitakachosafirishwa nje ya nchi kitatokana na mahitaji ya soko huria ambalo lipo Falme za Kiarabu, Oman, Qatar, Saudi Arabia, China, Indonesia, Vietnam na Malaysia.

Usafirishaji wa nyama na bidhaa zake kutoka kiwanda cha Tanchoice utakuwa wa magari maalum au kontena hadi uwanja wa ndege au bandarini.

Bidhaa za nyama zitasafirishwa kutoka Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Julius Nyerere wakati iliyogandishwa itasafirishwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Mradi huo utaajiri zaidi ya watu 500 ajira za moja kwa moja na kutengeneza nyingine nyingi zisizo za moja kwa moja.

Kiwanda cha Tanchoice kinatarajiwa kuendeleza wafanyakazi wake katika ujuzi wa kuchakata nyama, mafunzo ambayo yatatolewa ndani kwa ndani.

# Muswada wa kinga wakosolewa zaidi

**Na Elizabeth Zaya**

ASASI za kiraia zimesema marekebisho mengi yanayopendekezwa katika muswada wa marekebisho ya sheria mbalimbali namba 3 ya mwaka 2020, una athari na hatari kubwa zinazoweza kutokea iwapo utapita bila kuboreshwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwenye vyombo vya habari na asasi hizo ikiwamo Centre for Strategic Litigation, JamiiForums, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Baraza la Habari Tanzania (MCT), Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) na Twaweza, marekebisho mengi yanayopendekezwa yanakiuka maana na dhamira ya Katiba ya nchi.

"Sisi, asasi huru za kiraia tunaotetea na kuenzi misingi muhimu ya uhuru na demokrasia, tungependa kuikumbusha jamii nzima kuhusu athari zinazoweza kutokea iwapo Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali No. 3 (2020) utapita bila kuboreshwa."

Mapendekezo haya yanahatarisha misingi muhimu ya Katiba kama vile usawa mbele ya sheria (Ibara ya 13), Katiba kuwa ndio sheria kuu (Ibara ya 26), na mgawanyo wa madaraka baina ya mihimili ya dola (Ibara ya 4).

"Ibara ya 13-usawa mbele ya sheria uko hatarini. Katiba inatamka kwamba watu wote ni sawa mbele ya sheria, wanayo haki, bila ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria."

Kwa mujibu wa asasi hizo, marekebisho yanayopendekezwa kwenye Sheria ya uendeshaji wa Mahakama sura ya 237 yanaweka kinga dhidi ya kushtakiwa kwa watendaji wote katika mfumo wa mahakama kwa matendo waliyofanya kwa nia njema wakati wa ajira zao.

Walisema maboresho ya sheria kuhusu ajali mbaya na masharti mengineyo sura ya 310 na sheria ya utekelezaji wa haki na wajibu wa msingi, sura ya 3.

Pia,inasema yanasema mashtaka yote dhidi ya Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Spika, Naibu Spika au Jaji Mkuu hayawezi kuletwa moja kwa moja dhidi yao bali mshtaka hayo yanatakiwa kuletwa dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

"Kwa kuwalinda watu wenye nyadhifa hizo dhidi ya kushtakiwa mahakamani, marekebisho haya ya sheria yanadhoofisha uwajibikaji nchini."

"Zilisema uzoefu toka nchi nyingine duniani umeonesha kuwa, mara nyingi wahusika wanapowajibishwa wao wenyewe moja kwa moja huwa wanakuwa makini katika utendaji wao kuepusha makosa yasiyokuwa ya lazima,"walisema.

Aidha, walisema dhana ya usawa mbele ya sheria kama ilivyobainishwa kwenye Katiba inataka kwamba, kila mmoja bila kujali hadhi au nafasi yake, anatakiwa kuwajibishwa mbele ya sheria.

"Marekebisho haya yanaweka upendeleo kwa kuzingatia hadhi na nyadhifa za wahusika pindi wanapokiuka Katiba na Sheria tofauti na dhana ya usawa wa watu wote mbele ya sheria inavyoelekeza."

"Hakuna mantiki ya kuwaongezea kinga kwa sababu Katiba na sheria ya Mahakama tayari zinatoa kinga za kutosha za kuwawezesha watendaji hawa kutekeleza majukumu yao. "

Kadhalika, walipendekeza marekebisho sheria ya utekelezaji wa haki na wajibu wa msingi sura ya 3 yanaelekeza kwamba wanaoweza kufungua kesi za kikatiba ni wale tu ambao wameathiriwa moja kwa moja na swala husika.

Walisema kuondoa haki ya raia kufungua mashtaka mpaka tu pale ambapo wanakuwa wameathiriwa moja kwa moja inaondoa haki ya kisheria ya raia na taasisi kufungua mashtaka kwa maslahi ya umma.

"Kwa maelezo haya, ni dhahiri kwamba mapendekezo ya marekebisho ya sheria mbalimbali ni hatari sana kwa ustawi wa Jamhuri yetu ya Muungano. Tunawahimiza watunga sheria, vyombo vya habari, asasi za kiraia na wananchi wote kwa ujumla kuungana kupinga marekebisho haya hatarishi."

"Kwa kufanya hivyo, tutatimiza jukumu letu adhimu la kuilinda na kuiheshimu Katiba na pia kuendelea kujenga taifa letu kwa misingi ya demokrasia na utawala wa sheria."



Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia, akizungumza na wanachama wapya pamoja wa zamani wa chama hicho, jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Takukuru yaeleza sababu kuwahoji vigogo Chadema

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru), imeanza kuwahoji wabunge 69 wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na waliowahi kuwa wanachama wa chama hicho kuhusu ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka.

Waliotakiwa kuhojiwa jana ni pamoja na Mwita Waitara (Ubungo), Anthony Komu (Moshi Vijijini), Peter Lijualikali (Kilombero), Sesil Mwambe (Ndanda), Joseph Selasini (Rombo), Marwa Chacha (Serengeti), Pauline Gekul (Babati mjini) na James Millya (Simanyiro), lakini mahojiano yao yaliahirishwa kutokana na dharura ambayo haikuelezwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisa Uhusiano wa Taasisi hiyo, Doreen Kapwani, mahojiano hayo yanafanyika katika Ofisi za Takukuru Makao Makuu jijini Dodoma kuanzia jana na yanatarajia kukamilika wiki ijayo.

"Kwa taarifa hii, tunapenda kuuthibitishia umma kwamba ni kweli kuwa Takukuru makao makuu imewaita waheshimiwa wabunge wa Chadema, na waliowahi kuwa wabunge wa chama hicho kwa ajili ya mahojiano," alisema.

Alisema hatua hiyo inafanyika ikiwa ni mwendelezo wa uchunguzi unaoendeshwa na Takukuru, Makao Makuu wa malalamiko dhidi ya matumizi ya fedha za chama hicho na hatua iliyopo sasa ni ya kuwahoji wabunge 69, wanachama na waliowahi kuwa wanachama wa chama hicho.

Ofisa huyo alisema fedha hizo ni zile zilizolalamikiwa na waliokuwa wabunge wa chama hicho ambao walitangaza kukihama chama hicho, ambao katika malalamiko yao walidai kwamba walikuwa wakikatwa katika mishahara yao kila mwezi kuanzia Juni 2016.

"Kwa mujibu wa malalamiko hayo kila mwezi wabunge wa viti maalum walikuwa wakikatwa kiasi cha Sh. 1,560,000 na wabunge wa kuchaguliwa kwenye majimbo walikuwa wakikatwa Sh. 520,000 na kwamba hawakuwa wakifahamu namna fedha hizo zimekuwa zikitumika," alisema.

Aliongeza: "Tunapenda kujulisha umma kwamba, kama ambavyo Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru Brigedia Jenerali Mbungo, alivyoviambia vyombo vya habari Mei 27, 2020 ni uchunguzi dhidi ya tuhuma hii tayari ulishaanzishwa na baadhi ya wahusika walishaanza kuhojiwa."

Alisema, wanafanya hivyo kwa kuwa yawezekana katika tuhuma hiyo kukapatikana makosa, ikiwamo ubadhirifu na ufujaji wa fedha za chama na matumizi mabaya ya mamlaka.

"Makosa haya yote yanaangukia katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007 ambayo ndiyo inayoongoza chombo chetu," alisema.

Alisema mpaka sasa tayari wamefanya mahojiano na viongozi wa Chadema, viongozi waliowahi kuwa Chadema, wabunge waliotoa taarifa na maofisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

"Wengine ni viongozi wa Bodi ya Wadhamini wa Chadema na sasa wanawahoji, wabunge wanachama wa Chadema, pamoja na wabunge waliowahi kuwa na wanachama wa chama hicho," alisema.

# Ndalichako aifunda Bodi Veta

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, ameiagiza Bodi mpya ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (Veta), kuhakikisha mafunzo ya ufundi stadi yanawafikia Watanzania wengi zaidi ili kutatua changamoto ya ajira kwa vijana na kuchochea kasi ya uanzishwaji wa viwanda nchini.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Bodi ya Nane ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, jijini Dar es Salaam, Prof. Ndalichako alisema elimu na mafunzo ya ufundi stadi ni moja ya maeneo muhimu yanayopaswa kupewa kipaumbele na kutiliwa mkazo zaidi katika kujenga uchumi wa viwanda ili kutimiza azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa Viwanda.

Prof. Ndalichako pia aliiagiza Bodi hiyo kusimamia kwa karibu utekelezaji wa miradi mbalimbali inayosimamiwa na Veta, ikiwamo ujenzi wa vyuo vya Veta vya wilaya 29 unaoendelea hivi sasa na uboreshaji wa vyuo vilivyopo kwa kukarabati na kujenga madarasa, karakana na mabweni zaidi ili kutoa fursa kwa Watanzania wengi hasa vijijini kupata mafunzo hayo muhimu.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Veta, Dk. Pancras Bujulu, alisema Bodi iliyomaliza muda wake Februari mwaka huu, ilikuwa na mafanikio mengi kwa kipindi chake cha miaka mitatu, ikiwamo ongezeko la vyuo vinavyotoa mafunzo ya Ufundi Stadi nchini kutoka 451 hadi 68.

Alisema pia vyuo vinavyomilikiwa na Veta vimeongezeka kutoka 29 hadi 41, kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi wa ufundi stadi kutoka 169,118 hadi 302,369 na kusimamia shughuli mbalimbali za ubunifu hadi kuzalisha bidhaa halisia ambazo baadhi yake zimeingia sokoni.

# Madereva Namanga walalamikia rushwa

**Na Elizabeth Zaya**

MADEREVA wanaotumia mpaka wa Namanga, wamelalamikia kero mbalimbali mpakani humo ikiwamo madai ya kuombwa rushwa na maofisa wanaosimamia upimaji wa corona upande wa Kenya ili wawavushe.

Kero hizo zilitolewa na madereva hao walipotembelewa na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, kuangalia changamoto wanazokumbana nazo.

Madereva hao walidai wamekuwa wakiombwa fedha kwa kiwango tofauti ili wawajazie fomu zinazoonyesha hawajaambukizwa corona ili waingie nchini humo.

"Tunaishi maisha magumu kutokana na hali inayojitokeza hapa mpakani, na kinachotusikitisha zaidi ni kwamba hatukubaliani na vipimo ambavyo tunapimwa upande wa pili wa Kenya," alisema mmoja wa madereva hao Abdallah Hassan.

Dereva mwingine, Japheth Jeremia, alisema mara nyingi wakipimwa upande wa Kenya bila kutoa kiwango cha pesa wanachoombwa na maofisa hao hupewa majibu yanayoonyesha wameambukizwa corona.

"Tukipimwa upande wa Kenya tunaambiwa tuna corona, na mimi ni mmojawapo nimepimwa na sasa hivi ni wiki ya pili nimeambiwa nina corona na nimepewa cheti," alisema Jeremia.

Aliongeza: "Kinachosikitisha, kuna mazingira ambayo yanafanywa na wale watu wanaosimamia kupima na kutoa majibu katika mpaka wa Kenya, ukifika pale wanakuambia kama ukiwa na Sh. 2,000 Kenya (Sh. 43,000) huna corona na wanakujazia mafaili unapita."

Amani Jerald, alisema ana wiki mbili sasa tangu apimwe katika mpaka huo wa Kenya na kuambiwa ana corona.

"Mimi mwenyewe nina wiki ya pili niko hapa, nilienda upande wa Kenya nikapimwa na kuambiwa nina corona, baada ya kufuata majibu pale tukawekwa pembeni, baadaye tukawafuata wanaotoa majibu pale, wakasema kama utakuwa na Sh. 3,000 ya Kenya ( Sawa na Sh. 64,000), hapo utavuka na mimi hapa siumwi na wala sina matatizo yoyote," alisema Jerald.

Akijibu malalamiko hayo, Dk. Mollel alisema wanachukua malalamiko ya madereva hao na watayashughulikia kulingana na maelekezo yaliyotolewa na marais wa pande zote.

"Tuko pamoja kushughulikia malalamiko yenu kuhakikisha yanatatuliwa, kuna maelekezo ambayo yameshatolewa na marais wetu wa Tanzania na Kenya, sisi kazi yetu ni kutafuta ufumbuzi wa hizo changamoto, mimi leo nimekuja kuwasalimia na kujua kinachoendelea, lakini serikali yenu inawapenda na inajitahidi kufanya kila kinachowezekana kuhakikisha changamoto hii inaisha," alisema Dk. Mollel.

Aliwataka madereva hao kuwa wavumilivu katika kipindi hiki ambacho serikali inatafuta utatuzi wa changamoto zao.

Kwa mujibu wa Dk. Mollel, changamoto iliyojitokeza katika mpaka wa Namanga ni suala mtambuka ambalo linahusisha wizara zaidi ya moja, huku akiweka wazi kuwa suala hilo lina uhusiano wa kibiashara na uchumi baina ya nchi hizo.



Wakazi wa Kijiji cha Likombora, wilayani Liwale, mkoani Lindi, wakisafisha eneo kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa mradi wa vyoo vya kisasa, maji na usafi wa mazingira katika Shule ya Msingi Likombora, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Mbunge CCM ahojiwa tuhuma rushwa

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), mkoa wa Morogoro, inaendelea na uchunguzi wa tuhuma za rushwa dhidi ya Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Christine Ishengoma na watu mbalimbali kuhusu tuhuma hizo.

Mkuu wa Takukuru mkoani hapo, Janet Machulya, alikiri kwa waandishi wa habari Taasisi hiyo kumchunguza mbunge huyo na kuonya watu wanaotarajia kugombea nafasi mbalimbali za kisiasa katika uchaguzi ujao kuachana na rushwa.

"Hii taarifa tunaishughulikia kama ilivyo taratibu na kwa kuwa taratibu hizi ni za kiuchunguzi, kile ambacho kitabainika Takukuru kwa mujibu wa miongozo na sheria, tutachukua hatua kulingana na ushahidi utavyopatikana....," alisema Machulya.

Kuhusu viongozi walio madarakani kukamilisha ahadi zao kwa wananchi kwa kuwapa chochote wapigakura wao, aliwaonya kuacha na kufuata taratibu kwa kuwa mchakato wa uchaguzi ni suala la haki.

Dk. Ishengoma anatuhumiwa mnamo Mei 25, mwaka huu, kuwakusanya wajumbe wa mkutano mkuu wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), Kiwanja cha Ndege, kutoka kata zote za Manispaa ya Morogoro na kuwapatia rushwa ya kuanzia Sh. 50,000 alizodai ni za chakula cha kuku na kuwaomba kumchagua tena katika nafasi hiyo. Maofisa wa Takukuru walimkamata yeye na baadhi ya wajumbe hao wakiwamo madiwani wa viti maalum.

Inadaiwa baada ya mahojiano ya awali na Taasisi hiyo na kuachiwa, mbunge huyo alikwenda tena kuwapa fedha wajumbe hao, ambao baadhi wanadaiwa kuzikataa na wengine kupokea kitendo kilichofanya aitwe na kuhojiwa tena, wakiwamo viongozi wa ngazi ya mkoa wa CCM na UWT.

Dk. Ishengoma ambaye aliwahi pia kuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, alipotafutwa kwa njia ya simu kuzungumzia tuhuma za madai ya awali, alikata simu kwa madai yuko bungeni licha ya kuombwa akimaliza kikao kuwasiliana na mwanahabari hakufanya hivyo.

Baada ya Takukuru kuzungumzia suala hilo, Dk. Ishengoma aliopigiwa tena kuzungumzia tuhuma hizo, hakupokea simu, badala yake alipokea simu ya mwanahabari wa chombo kingine cha habari na mwandishi alipojitambulisha, hakumpa nafasi ya kumuuliza maswali na kudai suala la Takukuru halipo na kukata simu, akidai alikuwa bungeni.

Taasisi hiyo pia imewaburuza Mahakama ya Hakimu MKazi Mkoa wa Morogoro, Diwani wa Kata ya Boma, Amir Nondo na washtakiwa wengine watatu, kwa tuhuma za makosa ya udanganyifu ambayo imedai kwa mujibu wa marekebisho yaliyofanywa na sheria namba tatu ya mwaka 2016, makosa hayo ni ya uhujumu uchumi.


**GSP AUCTION MART**

***KUMB No. TATA/2020/DM/005***

**GSP AUCTION MART** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na kampuni ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED** S.L.P 40780 Dar es salaam tunapenda kutangaza mnada wa hadhara wa kuuza Magari kwa njia ya mnada wa magari twaja hapo chini.Siku ya ijumaa tarehe 26/06/2020 mnada utaanza Saa 5:00 kamili asubuhi katika yadi ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED** iliyopo Dar es salaam vingunguti na Mwanza Sinai.

| CUSTOMER NAME | MODEL | VEH_NO | LOCATION |
|---|---|---|---|
| IVORY ANTONY NDAMBALILO | LPO 10.2T/52 | T364 DLT | DAR ES SALAAM |
| JAKOVIC GENERAL SUPPLIES LTD | LP 909 | T488 DNR | DAR ES SALAAM |
| JAMES ANTHONY MMASSY | LP 909 | T432 DPS | DAR ES SALAAM |
| LUSUBILO JOSEPH KAJANGE | LPK 813 | T791 DRD | MWANZA |
| MAJID AHMED IDD | Ultra Bus | T773 DQM | MWANZA |
| MAJID AHMED IDD | Ultra Bus | T613 DQF | MWANZA |
| TWAHIL ABDALLAH MPULUJI | LPO 10.2T/52 | T167 DPU | DAR ES SALAAM |
| CONSTANTINO MLAGALA MSONJELA | LP 909 | T881 DNQ | MWANZA |
| CONSTANTINO MLAGALA MSONJELA | LP 909 | T487 DNR | DAR ES SALAAM |
| ELIAS DEBLO ELIA | LPO 10.2T/52 | T906 DPK | DAR ES SALAAM |
| JUED HOMES LTD | LP909 Bus | T517 DNS | DAR ES SALAAM |
| JUED HOMES LTD | LP909 Bus | T207 DNS | DAR ES SALAAM |
| JUED HOMES LTD | LP909 Bus | T722 DNQ | MWANZA |
| JUED HOMES LTD | LP909 Bus | T814 DMQ | DAR ES SALAAM |
| ZAKARIA JUMA MAIGE | LP909 Bus | T328DRE | MWANZA |
| FILGONA RANGA DUKO | LP909 Bus | T178DPE | DAR ES SALAAM |
| FILGONA RANGA DUKO | LP909 Bus | T 526DNP | DAR ES SALAAM |
| THEOBALD NICAS MPIRI | LP909 Bus | T996 DPL | DAR ES SALAAM |
| DEOGRATIUS ORGENES LYMO | LP909 Bus | T813DQK | DAR ES SALAAM |
| SALVANUS JOHN CHIDOWE | LP909 Bus | T870 DPA | DAR ES SALAAM |
| JULIUS ELIZEI CHALAMILA | LP909 Bus | T196 DSB | MWANZA |
| MUSTAFA SAID MBINGA | LP909 Bus | T248DQN | DAR ES SALAAM |

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi anatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki ni juu ya mnunuzi.
5. Kwa yeyote atakayeharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:**
**GSP AUCTION MART PO BOX 310088 DAE ES SALAAM.**
**+255 654 922 892, +255 687 638 679**

115771502

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mkazo uwekwe kwenye makusanyo bajeti ijayo

**BAJETI** ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha inatarajiwa kuwasilishwa bungeni jijini Dodoma baadaye leo alasiri.

Mpango wa Maendeleo ya Taifa na ukomo wa bajeti ya mwaka 2020/21, unaonyesha bajeti hiyo inatarajiwa kuwa ya Sh. trilioni 34.88, huku Sh. trilioni 21.98 zikitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikiwamo gharama za uchaguzi mkuu wa Oktoba, mwaka huu.

Bajeti hiyo ya mwisho kwa awamu ya kwanza ya serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli, imeongezeka kutoka Sh. trilioni 33.1 zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha (2019/20), sababu kuu ikitajwa kuwa gharama za uchaguzi mkuu.

Mbali na uchaguzi mkuu, bajeti hiyo pia imezingatia mahitaji halisi ya ugharamiaji miradi mikubwa ya kimkakati, ulipaji mishahara, deni la serikali na vipaumbele vingine vya taifa.

Mpango uliowasilishwa bungeni Machi 11 mwaka huu, unabainisha kuwa kiasi cha Sh. trilioni 34.88 kinatachorajiwa kukusanywa, kinajumuisha mapato ya ndani ya Sh. trilioni 24.07 (asilimia 69 ya bajeti yote), mikopo ya ndani Sh. trilioni 4.9, mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara Sh. trilioni 3.04 na misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo Sh. trilioni 2.87.

Kwa mujibu wa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, kati ya fedha hizo, Sh. trilioni 21.98 zitakuwa za matumizi ya kawaida na Sh. trilioni 12.9 za matumizi ya maendeleo (asilimia 37 ya bajeti yote).

Bajeti ya maendeleo inajumuisha Sh. trilioni 10.16 ambazo ni fedha za ndani (asilimia 78.8 ya bajeti ya maendeleo) na Sh. trilioni 2.74 fedha za nje.

Pia Sh. bilioni 400 zitatumika kulipa madeni yaliyohakikiwa, ujenzi wa reli ya kati ya kisasa (SGR) Sh. trilioni 2.1, mradi wa umeme wa Julius Nyerere Sh. trilioni 1.6 na mingine ni Sh. trilioni 6.06.

Nipashe tunaipongeza serikali kwa jitihada zake katika kuongeza makusanyo na kudhibiti mianya ya ufujaji wa fedha za umma kwa lengo la kutekeleza miradi ya maendeleo.

Takwimu za makusanyo zinazotolewa na Mamlaka ya Mapato (TRA), zinaonyesha serikali ya awamu ya tano imefanikiwa kuongeza makusanyo kwa wastani Sh. bilioni 450 kwa mwezi.

Takwimu hizo zinaonyesha kuwa serikali imeongeza makusanyo kutoka wastani wa Sh. bilioni 850 kabla ya Novemba 2015 hadi kufikia Sh. trilioni 1.3 kwa mwezi.

Hata hivyo, pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali ya awamu ya tano kuimarisha makusanyo ya nchi kwa kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato, taarifa za kamati mbalimbali za Bunge na ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), zinaonyesha utekelezaji usioridhisha wa miradi ya maendeleo kutokana na ukosefu wa fedha.

Hii inatokana na ukweli kwamba kiwango kikubwa cha makusanyo kinatumika kulipa Deni la Taifa na mishahara ya watumishi wa umma.

Kwa mujibu wa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, serikali inatumia wastani wa Sh. bilioni 600 kulipa Deni la Taifa na Sh. bilioni 550 kwa mishahara ya watumishi wa umma kila mwezi, hivyo katika makusanyo yake ya Sh. trilioni 1.3, hubakiwa na Sh. bilioni 150 pekee.

Ni kutokana na hali hii, Nipashe tunaona ipo haja kuongeza juhudi zaidi katika ukusanyaji wa mapato ya nchi sambamba na kudhibiti zaidi mianya ya ubadhirifu, ili kutekeleza miradi muhimu kwa manufaa ya kizazi kiichopo na kijacho.

Mpango wa Maendeleo ya Taifa na ukomo wa bajeti ya mwaka ujao wa fedha unaonyesha asilimia 69 ya mapato yatategemea makusanyo ya ndani.

Kwa msingi huo, tunapoelekea kufunga mwaka wa fedha 2019/20 siku 19 zijazo, mamlaka zinazohusika na ukusanyaji wa mapato, zinapaswa kuhakikisha zinatatua matatizo yaliyojitokeza katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu, ili yasijirudie mwakani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



## Karibu Ruwasa tumtue ndoo mama, vichakani nako 'stop'

Na Sabato Kasika

**KATIKA** jitihada zake za kutaka Watanzania wote wanapata maji tena katika maeneo ya karibu, kwa lengo la kutaka adha ya kumtua mama ndoo kichwani itimie kwa vitendo, serikali ilianzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa), mwaka jana.

Ilianzishwa kwa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira na ikaanza kazi Julai mwaka jana.

Inaeleweka, huduma ya majisafi na salama ni nyeti, kwani kiafya asilimia 70 ya mwili wa binadamu unaundwa na maji, jambo linalouwezesha mwili kufanya kazi kwa usahihi.

Ni kawaida mwili unapokosa maji ya kutosha, iko wazi unakaribisha madhara mbalimbali ya muda mfupi na mrefu, ikiwamo magonjwa ya shinikizo la damu, saratani ya figo.

Kinachofanywa na Ruwasa kuhakikisha maji yanapatikana, inasanifu na kusimamia ujenzi wa miradi ya maji vijijini, inatafiti maji ardhini, kuchimba visima na kujenga mabwawa, kusajili na kuviwezesha vyombo vya watumiaji maji vijijini.

Ruwasa, pia inahamasisha sekta binafsi kushiriki katika maendeleo ya sekta ya maji vijijini, pia kumshauri Waziri wa Maji kuhusu uendeshaji sekta ya maji vijijini.

Serikali inafanya hayo kwa vile kuhakikisha maji yanapatikana, yana ubora, masafi na huduma za usafishaji, ni jambo muhimu linalopewa kipaumbele, ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma katika maeneo jirani.

Hivyo, Watanzania wanachopaswa kutambua ni kwamba, serikali ihakikishe kunakuwapo huduma na matumizi sahihi ya maji, yakiwa ni salama kwa ngazi zote, ikiwamo miundombinu yake.

Tafsiri ya usalama wa maji inaenda mbali hadi kwenye usimamizi wa majitaka. Hapo kuna suala la kuwapo vyoo sahihi na bora, badala ya tabia ya watu kujisaidia vichakani. Nchini Ziwa Victoria, katika baadhi ya maeneo kuna sifa hiyo, inayoishia kuchafua mazingira.

Baadhi ya watu wanaharibu vyanzo vya maji na miundombinu yake kwa kujisaidia kwenye vyanzo, hali inayochangia, kukwamisha huduma za maji kwenye jamii.

Huwa kuna tuhuma kwa baadhi ya watu wamekuwa wakijisaidia ndani ya Ziwa Victoria, tabia ambayo kimsingi, ni uchafuzi wa mazingira unaopaswa kuachwa kulinda afya za umma kwa jumla.

Mathalan, Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, anasema Ruwasa imepanga kufanya usanifu wa Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria, katika vijiji anavyovitaja ni kuanzia Chumwi kwenda vijiji vya Mabui Merafuru, Mikuyu na Seka.

Dk. Anney anasema ni mradi utakaohusisha uchimbaji visima na kufunga pampu za mkono, pia watapanua mradi huo wa maji kwa ajili ya vijiji anavitaja; Bulinga/Bujaga kwenda vijiji vya Bugunda na Kome.

Mbali na kujipanga kwa vijiji vimgine kadhaa, Ruwasa inalenga kukarabati visima 10 vyenye pampu za mkono.

Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), zinasema umuhimu huo wa maji unawafikia takribani watu bilioni 2.2 duniani wanaokosa maji salama ya kunywa na wengine bilioni bilioni 3 hawana huduma za msingi za sehemu za kunawa mikono.

Kutokana na hali hiyo, mashirika hayo yanasema majisafi na salama ni ndoto kwa watu wengi duniani.

Pia, ripoti imebaini hatua kubwa zilizopigwa katika kufikia fursa ya msingi ya maji kwa wote, usafi na huduma za kujisafisha, pengo kubwa liko katika ubora wa huduma zinazotolewa.

Inaelezwa kupitia ripoti kwamba, suala la watu kujisaidia haja kubwa hadharani vimepunguzwa kwa nusu tangu mwaka 2000 kutoka asilimia 21 hadi asilimia tisa, wahusika duniani, kwa maana ya jumla ya watu milioni 673.

Vitendo hivyo vinatajwa kuibebesha serikali mzigo mkubwa na kwamba katika nchi 39 nyingi zikiwa Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, wanaojisaidia hadharani wameongezeka.

Hiyo inajenga maana kwamba, kunahitajika hatua za kuunga mkono juhudi ambazo serikali imekuwa ikichukua kuhakikisha Watanzania wanapata majisafi na salama.

Pia, umma unaopaswa kujiepusha na vitendo vya kujisaidia sehemu ambayo siyo rasmi na wakavilinda vyanzo vya maji na miundombinu yake.

# CCM yafungua milango mchakato wa ndani

**Na Elizabeth Zaya**

HALMASHAURI Kuu ya Taifa ya CCM, jana, ilijadili Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu, na kuelekeza kutolewa kwa ratiba ya mchakato wa ndani wa uteuzi wa wanachama wanaoomba kupewa dhamana ya uongozi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Humphrey Polepole, kikao hicho kilifanyika jijini Dodoma chini ya Mwenyekiti wake Rais John Magufuli.

Alisema pamoja na mambo mengine kikao hicho kilipokea na kujadili mpango wa maandalizi ya uchaguzi mkuu wa Oktoba, mwaka huu na kwamba iliridhishwa na maandalizi yaliyofanyika.

"NEC imepokea na kujadili mpango wa maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu. Kwa kauli moja imeridhishwa na kiwango cha maandalizi ya kuelekeza huo na kuelekeza kutolewa mara moja kwa ratiba ya mchakato wa ndani wa uteuzi wa wana CCM wanaoomba kupewa dhamana ya uongozi katika vyombo vya dola," alisema Polepole.

Aidha, alisema pia ilipokea taarifa ya maendeleo ya uandishi wa mwelekeo wa Sera za CCM kwa Mwaka 2020-2030 na kujiridhisha kuwa kazi nzuri imefanyika mpaka ngazi ya rasimu ya pili.

Alisema ilipitia kwa mara ya pili taarifa ya uandishi wa ilani ya CCM katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu na kuipongeza Sekretarieti ya Halmashauri Kuu Taifa kwa kujumuisha maoni ya wadau mbalimbali na kuelekeza maandalizi ya mwisho, ili ilani hiyo iwasilishwe katika Kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa kwa uamuzi wa mwisho.

Aidha, alisema ilipokea taarifa ya serikali juu ya mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona na hatua ambazo zimechukuliwa kuukabili ugonjwa huo kwa mafanikio makubwa nchini.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC), James Mataragio, akizungumza wakati wa uzinduzi wa kituo cha mafuta cha TANOIL, katika Kata ya Segera, wilayani Handeni, jana. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigella. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

## Mtumishi kortini madai kusambaza picha za ngono

**Na Hellen Mwango**

MTUMISHI wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sadiki Senge (46) maarufu kama Graffiti de Thiago, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu akikabiliwa na shtaka la kusambaza picha za ngono kwa njia ya mtandao wa WhatsApp.

Mshtakiwa huyo alisomewa shtaka lake mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kati ya Julai 11, 2019 na Mei 5, mwaka huu jijini Dar es es Salaam, mshtakiwa alitumia mfumo wa kompyuta kusambaza picha za ngono kupitia mtandao wa WhatsApp.

Mshtakiwa alikana shtaka hilo.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika uliomba tarehe ya kumsomea maelezo ya awali.

Hakimu Chaungu alisema mshtakiwa atasomewa maelezo ya awali Julai 14, mwaka huu.

Mshtakiwa yuko nje kwa dhamana ya wadhamini wawili akiwamo mmoja kutoka serikalini, waliotoa saini hati ya dhamana ya Sh. milioni 20 kila mmoja.

# Waziri aagiza mkurugenzi kukamatwa

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira, Anthony Mavunde, ameagiza Idara ya Uhamiaji nchini kumzuia kutoka nje ya nchi Mkurugenzi wa Kampuni ya Knight Support, Bresing Kachambwa, kwa kushindwa kupeleka makato ya wafanyakazi zaidi ya Sh. bilioni 8.417.

Akizungumza na Menejimenti ya NSSF na uongozi wa Kampuni ya Ulinzi ya Knight Support, jana jijini Dar es Salaam, alisema ameiandikia barua Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kusaidia upatikanaji na kumleta nchini Mama Christin ambaye ana hisa nyingi kwenye kampuni hiyo.

Mavunde alisema kumekuwapo na kesi ya muda mrefu ya wafanyakazi wa Knight Support na kwamba tayari NSSF ilichukua hatua za awali baada ya madai ya muda mrefu ya wafanyakazi ndipo kampuni hiyo ilipopelekwa mahakamani.

Alifafanua kwamba Mahakama ilitoa hukumu yake, na NSSF ilipaswa kukaza hukumu kwa ajili ya kukamata mali za mwajiri ili waweze kufidia michango ambayo haijawasilishwa ambayo jumla yake ni Sh. bilioni 8.417 inayojumuisha michango na tozo za adhabu.

Kwa mujibu wa Mavunde, baada ya hukumu NSSF walikwenda kukamata mali za mwajiri, lakini kampuni ilibainika haina mali yoyote kwa sababu zilizokuwapo zilikuwa hazina jina la kampuni hiyo.

Alisema wahusika wa kampuni hiyo wote hawapo, na sasa amebakia mkurugenzi ambaye hawezi kujitoa kwamba sio sehemu ya kampuni na sheria inasema vizuri.

Alisema serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na menejimenti mpya ya NSSF ambayo katika kipindi cha muda mfupi imeongeza makusanyo kutoka Sh. bilioni 58 kwa mwezi mpaka kufikia zaidi ya Sh. bilioni 100 kwa mwezi.

Aidha, alisema: "Naagiza kuanzia leo (jana) waajiri wote ambao wanajua kabisa kwamba kuna michango ya wafanyakazi haijawasilishwa NSSF ni bora wajisalimishe mapema mbele ya shirika kwa sababu hatua zitakazo chukuliwa sasa ni kuwakamata waajiri hao ili wafanyakazi wapate stahiki zao kwa mujibu wa sheria."

Waziri Mavunde alisema kumekuwapo na wimbi kubwa la waajiri kufikiria kwamba wanaweza kufanya mzaha na maisha ya watu ambao sheria na Katiba imetamka kwamba wapelekewe michango yao NSSF.

Aliwataka waajiri wote nchini kuzingatia matakwa ya sheria yanavyoelekeza kuhusu michango ya wafanyakazi ambayo ni haki yao ya kimsingi kuwasilishwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa madhumuni ambayo yamesemwa katika ibara ya 11 ya Katiba.

"Lengo kubwa ni kwamba mfanyakazi baada ya kufanyakazi kwa muda mrefu basi ile michango yake imfae na kumsaidia atakapostaafu," alisema.

Alisema haiwezekani mfanyakazi mshahara wake ukaupunguza kwa mujibu wa sheria, halafu makato anakaa nayo mwajiri anayazungusha kwamba jambo hilo ni dhambi kubwa na serikali haiwezi kuliruhusu.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa MSSF, William Erio, alisema kampuni hiyo ilikuwa haijawasilisha michango ya wafanyakazi wake kuanzia Julai mwaka 2011.

Alisema baada ya kushinda kesi kampuni hiyo ilitakiwa kulipa NSSF Sh. milioni 60 kila mwezi, lakini hawakutekeleza na hivyo shirika lililazimika kuchukua hatua za ziada ya kukazia hukumu.

Erio alisema miongoni mwa hatua walizotaka kuchukua ni kukamata mali za kampuni ili tuweze kuuza na kuwalipa wafanyakazi hao, lakini hawakufanikiwa kupata mali yoyote.

"Tulishangaa kuona hata magari yaliyoandikwa Knight Support pia wamekodi na ukisoma kadi za usajili wa magari sio wamiliki wa magari husika," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo waliiandikia barua Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ili kusaidia kurejeshwa nchini mmiliki, Christina Angelah, ambaye ni raia wa Uingereza na Kenya aweze kurejeshwa nchini ili ajibu tuhuma zake.

Naye, Kamishna wa Kazi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Brigedia Jenerali Francis Mbindi, amewaelekeza maofisa kazi wote nchini kuhakikisha waajiri wote wanatekeleza na kuzingatia sheria za kazi.

# Watoto wauawa kwa mapanga

**Na Mwandishi wetu**

WATOTO wawili wa miaka minne wameuawa mkoani Pwani na Shinyanga, kwa kukatwa katwa kwa mapanga.

Katika tukio la Pwani, mtoto mmoja aliuawa kwa kukatwa kwa mapanga kwa kilicholezwa ni wivu wa mapenzi kwa mke mkubwa kukosa mtoto wakati mke mdogo ana mtoto.

Kamanda wa Polisi mkoani Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema tukio hilo lilitokea Juni 2, mwaka huu, majira ya saa 3 usiku eneo la Mji Mpya Kata ya Kisutu wilayani Bagamoyo.

Alisema mtoto huyo alikuwa na bibi yake Clemencia Mashaka (65) alipigiwa simu na namba ambayo haikufahamika, akielezwa kuwa kuna dereva pikipiki atamfuata ili ampeleke eneo la Kingani kumpa huduma mgonjwa aliyedaiwa mimba yake kuharibika.

Alisema mtu huyo alifika na kumchukua bibi na mjukuu wake na walipofika porini, dereva alisimamisha pikipiki yale na kuanza kuwakatakata na mapanga bibi na mjukuu na kusababisha kifo cha mtoto Joshua Emmanuel na majeraha kwa bibi Clemensia.

Kamanda Nyigesa aliwataja wanaoshikiliwa ni Hussein Chongo (21) dereva pikipiki mkazi wa Kimara Ng'ombe Bagamoyo, Sofia Marius (28), mkazi wa Nianjema Bagamoyo na Sofia Roman (23) wakala wa mitandao ya simu mkazi wa Mbagala jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Kamanda huyo, chanzo cha mauaji ni wivu wa kimapenzi, kwa Sofia Marius ambaye ameolewa ndoa ya wake wawili na hajabahatika kupata mtoto, huku mwenzie akiwa na mtoto Joshua, hivyo kufanya njama za mauaji ya mtoto huyo.

Wakati huo huo, Mtoto Emmanuel John (4), mkazi wa Ndala Manispaa ya Shinyanga, anadaiwa kuuawa na mjomba wake, James Mhoja (36), kwa kuchinjwa shingoni na kutenganishwa kichwa na kiwiliwili.

Kaka wa marehemu, Godfrey Mhoja, alisema lilitokea juzi majira ya mchana, wakati marehemu akicheza na wenzake, ndipo alipofika mjomba wao akiwa na mapanga mawili na rungu, akamshika na kuanza kumchinja shingo.

Alisema wakati akimchinja shingo ndipo akasikia kelele ikabidi atoke nje na kumuona mdogo wake akiwa amelala chini, huku akitoka damu shingoni, na alipomzuia mjomba wao huyo alimkimbiza na yeye na mapanga.

Alisema alikimbilia ndani na baada ya hapo ilibidi aruke ukuta kisha kwenda kuomba msaada kwa majirani.

"Tulivyokuja na majirani kutoa msaada tulikuta mdogo wangu akiwa ameshachinjwa shingo na kutenganishwa na kiwiliwili, huku mjomba akianza kututishia kutukata mapanga, lakini wananchi walianza kumshambulia kwa kumpiga mawe na yeye akafariki papo hapo,"alisema Mhoja.

"Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Joseph Paulo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa chanzo cha mauaji hayo wanakichunguza.

**Imeandikwa: Julieth Mkireri (PWANI) na Marco Maduhu (SHINYANGA)**




Meneja Biashara wa Kampuni ya Yara Kanda ya Ziwa, Phillipo Mwakipesile (kulia), akimwonyesha mmoja wa mawakala wa kampuni hiyo, Luta Juma, namna ya kutumia kitakatishi ikiwa ni sehemu ya makabidhiano ya vifaa vya kujikinga na Covid-19 kwa mawakala na wakulima. Wengine ni mwakilishi wa wakulima kutoka Urambo, Ibrahim Kagete na mmoja wa mawakala kutoka Tabora, Secilia Lyakurwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Bunge lapitisha muswada unaomkinga Rais kushtakiwa

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

BUNGE limepitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2020, ambao pamoja na mambo mengine, unapendekeza mashauri yote ya madai dhidi ya viongozi wakuu wa nchi yafunguliwe dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Akisoma maelezo ya muswada huo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelardus Kilangi, aliliambia Bunge jana kuwa lengo la marekebisho hayo ni kukidhi maudhui ya dhana ya kinga ya mashtaka dhidi ya viongozi hao.

Profesa Kilangi alibainisha kuwa muswada unalenga kufanya marekebisho ili kuweka masharti yatakayotaka mtu yeyote anayekusudia kufungua shauri lolote la kikatiba chini ya Ibara za 12-29 zinazohusu haki za msingi, kuidhihirishia mahakama ni kwa kiasi gani mlalamikaji ameathiriwa na ukiukwaji wa haki anayolalamikia.

Profesa Kilangi alisema marekebisho ya Sheria ya Masuala ya Rais, Sura ya 9, yanalenga kurekebisha katika Kifungu cha 6 ili mashauri dhidi ya Rais kwa mambo anayodaiwa kuyatenda yeye binafsi kama raia yaliyoruhusiwa kufunguliwa dhidi yake kwa mujibu wa Ibara ya 46(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yafunguliwe baada ya kutoka madarakani.

"Kifungu cha 7 kinapendekezwa kurekebishwa ili mashauri yoyote dhidi ya Rais yafunguliwe dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Lengo la marekebisho haya ni kuwa na maudhui ya dhana ya kinga dhidi ya Rais ambayo ni kulinda hadhi ya Rais na nafasi yake," alisema.

# Wakulima washukuru msaada vifaa corona

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAKULIMA na mawakala wa Kanda ya Ziwa wanaotumia mbolea ya Kampuni ya Yara wameipongeza kampuni hiyo kwa kuwajali na kuhakikisha wanaendelea na shughuli za kilimo kwa kuwapa vitakatishi vya kujikinga dhidi ya homa ya Covid-19.

Akizungumza kwa niaba ya wakulima hao, Ibrahim Kagete kutoka Urambo, ambaye pia alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, alisema wamefanya jambo la kuigwa kwani wakulima na mawakala sasa wataweza kufanya shughuli zao kwa uhakika kwani Covid-19 ni tishio.

"Maambukizo yamepungua kwa kiasi kikubwa, lakini lazima tuendelee kuchukua tahadhari. Walichokifanya Yara leo ni heshima kubwa kwa wakulima na mawakala kwani hawa ndio wazalishaji wa chakula ambacho kinategemewa ndani na nje ya nchi," alisema.

Alitoa changamoto kwa mawakala waliohudhuria shughuli hiyo ya ugawaji wa vitakatishi kuhakikisha vifaa hivyo vinawafikia wakulima wote katika maeneo yaiyoelekezwa na kampuni hiyo ili waweze kujikinga ipasavyo huku wakiendelea na shughui zao za kilimo.

"Kuna wakulima ambao hawafahamu chochote kuhusu Covid-19 nendeni mkawaelimishe, lakini pia muwape vifaa hivi vya kujikinga ili wawe salama," alisema.

Meneja Biashara wa YARA Kanda ya Ziwa, Phillipo Mwakipesile, alisema vifaa saidizi vilivyotolewa ni vitakatishi, huku akibainisha kuwa kampuni hiyo imetumia Sh milioni 82 kwa vifaa hivyo katika kanda tatu ambazo ni Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa.

"Wakulima wanalo jukumu la kuendelea kuzalisha chakula huku wakiendelea kujikinga ili kuepusha uwezekano wa janga la njaa kutokana na ugonjwa huu wa homa ya mapafu," alisema.

**Maambukizo yamepungua kwa kiasi kikubwa, lakini lazima tuendelee kuchukua tahadhari. Walichokifanya Yara leo ni heshima kubwa kwa wakulima na mawakala kwani hawa ndio wazalishaji wa chakula ambacho kinategemewa ndani na nje ya nchi**

# Madiwani wataka mapato hifadhi

**Na Welingtone Masele,** SIKONGE

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge mkoani Tabora, limeagiza uongozi wa Jumuiya ya Hifadhi Wanyamapori Ipole (Juhiwai), mapato yote yanayokusanywa yanadhibitiwa ili kuinufaisha jamii inayoizunguka hifadhi hiyo na wananchi wa wilaya hiyo.

Diwani wa Kata ya Ipole, John Mbogo, alisema inasikitisha kuona jumuiya iliyoanzishwa na wananchi na kupewa dhamana ya kusimamia eneo hilo haiwanufaishi wanachama wake.

Alisema jumuiya hiyo inakusanya fedha nyingi kutoka kwa wananchi, lakini haijulikani fedha hizo zinakwenda wapi au zinatumika kwa kazi gani na hata udhibiti wake unatia mashaka.

Diwani wa Kata ya Mpombwe, Juma Mdullah, alisema uwapo wa jumuiya hiyo ni muhimu katika wilaya hiyo, lakini kuna changamoto zake na kwamba iliundwa kamati ya uchunguzi ambayo ilibainisha kasoro za kiutendaji ikiwamo matumizi mabaya ya fedha.

Akitoa ufafanuzi wa suala hilo, Mkuu wa wilaya hiyo, Peresi Magiri, alisema jumuiya zote za hifadhi ya wanyamapori zinazoanzishwa na jamii zinapaswa kuwanufaisha wananchi wa eneo husika na sio viongozi kujinufaisha wenyewe.

Kadhalika, alisema jumuiya hizo zina utaratibu wake wa uendeshaji ikiwamo ukusanyaji mapato na haziingiliwi na mtu, hata hivyo haiwapi mamlaka ya kufanya kila kitu watakavyo, isipokuwa kwa kufuata taratibu zilizowekwa na serikali.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Mwalimu Peter Nzalalila, alisisitiza kuwa serikali ilishaelekeza taasisi zote kutumia mashine ya 'POS' katika kukusanya mapato kutoka kwa wananchi ili kuepusha udanganyifu.

"Naagiza kuanzia sasa mapato yote Juhiwai yakusanywe kwa kutumia mashine za 'POS' ili kuepusha wizi, tunataka ijulikane kila mwaka wanakusanya kiasi gani na halmashauri inapata kiasi gani," alisema.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa huo, Robert Makungu, alisema jumuiya nyingi za uhifadhi wanyamapori hali si shwari na kuahidi kufuatilia taratibu za uendeshaji wake kwenye mamlaka husika.



Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete, akimsikiliza Meneja wa Benki ya Stanbic tawi la Makao Makuu, Richard Chenga, wakati akikabidhi mchango wa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 9.4 kutoka benki hiyo kwa ajili ya Kituo cha Afya Miono. Vifaa tiba hivyo ni sehemu ya mchango wa benki hiyo katika kuunga mkono jitihada za serikali kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora za afya. Wa kwanza kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chalinze, Zainabu Makwinya na Diwani wa Miono, Juma Mpwimbwi (wa pili kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maji yamnyima usingizi Kanyasu

**Sara Magesa,** GEITA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amesema hakuna jambo lililomnyima usingizi kama changamoto ya upatikanaji wa majisafi katika mji wa Geita.

Kanyasu ambaye ni Mbunge wa Geita Mjini, wakati anaingia jimboni humo upatikanaji wa maji ulikuwa asilimia 15, huku akitumia sehemu kubwa ya michango yake bungeni kuzungumzia upatikanaji wa huduma hiyo ambayo kwa sasa ni asilimia 57 hadi 60.

Alisema mji huo unaokadiriwa kuwa na watu zaidi ya 300,000 umetengewa Sh. bilioni 100 kwa ajili ya mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria utakaoufanya mji huo, kuwa na maji kwa asilimia 100.

Alisema alipoingia madarakani kwa kushirikiana na halmashauri ya mji waliweka kipaumbele cha kuboresha sekta ya elimu na afya na kwa kipindi cha miaka mitano wamejenga shule za msingi mpya 13 na sekondari saba.

Alisema katika sekta ya afya, zahanati 23 zimekamilika huku nyingine tatu ujenzi ukiendelea na fedha zilizotumika ni za miradi ya maendeleo ya jamii (CSR) kutoka halmashauri, mbunge na nguvu za wananchi.

Pia, alisema huduma ya umeme na miundombinu ya barabara imeboreshwa ikilinganishwa na miaka mitano iliyopita na kwamba hakuna anayeweza kukamilisha vitu vyote kwa asilimia 100 kwa kipindi cha miaka mitano.

Baadhi ya wananchi akiwamo Shija Fundikira, alisema jimbo hilo lilikuwa na changamoto kubwa ya majisafi na kupitia mbunge huyo serikali imetoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji ambayo yameondoa adha ya maji kwa wananchi.

Ikorongo Otto, alisema baadhi ya ahadi alizotoa Kanyasu ni pamoja na kutatua changamoto ya umeme na miundombinu ya barabara ahadi ambazo zimetekelezwa kwa kiwango kidogo na kwamba wanahitaji mtu atakayehakikisha kero hizo zinamalizika.

## Hatimaye Uvinza yapata hospitali

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

MKUU wa Wilaya ya Uvinza, Mwanamvua Mrindoko, amezindua utoaji huduma za afya katika Hospitali ya Wilaya ya Uvinza, utakaosaidia wananchi hususani wajawazito kuepuka adha ya kusafiri kilomita 300 kupata huduma katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kigoma, Maweni.

Akizungumza juzi wakati wa uzinduzi wa hospitali hiyo iliyogharimu Sh. bilioni 1.5, Mrindoko alisema huduma za afya katika wilaya hiyo zilikuwa zikiishia ngazi ya kituo cha afya, hivyo kusababisha wananchi wenye mahitaji ya huduma za ngazi ya hospitali ya wilaya kulazimika kusafiri kufuata matibabu kwenye hospitali ya rufani ya mkoa huo.

"Hii ni hatua kubwa sana kwenye wilaya hii, kwa sababu hakukuwa na hospitali ya wilaya, hivyo ililazimu mtu kusafiri umbali mrefu kwa mujibu wa wilaya yetu kuna mtu anatembea zaidi ya kilomita 360 kufika Maweni," alisema.

Naye Mganga Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Reuben Mwakilima, alisema hospitali hiyo imeanza kutoa huduma za baba, mama na mtoto, vipimo vya maabara, wagonjwa wa nje na wajawazito kujifungua.

## Waziri amsimamisha kazi Mkurugenzi KIA

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, amemsimamisha kazi, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Uendeshaji na Uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), Martin Kinyamagoha, kuanzia jana.

Waziri Kamwelwe amesema ametengua uteuzi wake baada ya kushindwa kutekeleza vyema majukumu yake katika kipindi kifupi tangu ateuliwe kushika nafasi hiyo.

Kamwelwe alisema ametengua uteuzi wake kwa sababu hawezi kuendana na kasi ya kufunguliwa kwa milango ya kuanza kuingia watalii nchini.

## Wanolewa kutambua viuatilifu vya mimea

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

WAFANYABIASHARA wa pembejeo za kilimo na mifugo zaidi ya 68 kutoka mikoa ya Ruvuma, Lindi, Mtwara na Pwani, wameanza kupatiwa mafunzo ya taaluma maalumu ya viuatilifu na udhibiti endelevu wa visumbufu vya mimea.

Mafunzo hayo ya siku tano yaliyotolewa na Taasisi ya Udhibiti wa Viuatilifu ukanda wa Kitropikali nchini (TPRI), yakilenga wauzaji na wamiliki wa maduka ya pembejeo yanayouza viuatilifu kwa wakulima.

Mratibu wa mafunzo hayo kutoka TPRI nchini, Jumanne Rajabu, alisema utafiti uliofanywa na taasisi hiyo wamebaini kuwa wafanyabiashara wengi wa maduka ya pembejeo za kilimo wanauza viuatilifu batili na vilivyopita muda wake jambo ambalo ni hatari kwa usalama wa mazao ya mkulima kutokana na wengi wao mazao yao kupata athari mbalimbali.

## HABARI BUNGENI



# Fidia barabara Tamco-Mapinga kulipwa kwa awamu

BUNGE limeelezwa kuwa fidia katika barabara ya Tamco- Mapinga ya zaidi ya Sh. bilioni 8.9 italipwa kwa awamu katika maeneo ambayo kazi ya ujenzi inafanyika.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Mary Muro, aliyehoji mchakato wa ulipaji fidia kwa wananchi hao waliopisha mradi.

"Ni lini wananchi wa Kibaha waliopisha ujenzi wa barabara Tamco-Mapinga watalipwa fidia,"alihoji.

Ikijibu, wizara hiyo ilisema jumla ya Sh. milioni 989.863 zilizotengwa kwa ajili ya fidia ya kilometa tano za mwanzo zimeshapokelewa na utaratibu wa kuwalipa wananchi fidia unaendelea.

Ilisema kiasi cha Sh. milioni 32.068 kimelipwa kwa wananchi ili kupisha eneo la ujenzi wa kilometa mbili zilizoanza kujengwa katika mwaka wa fedha 2018/19 na kazi zinaendelea.

Ilieleza katika mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya mita 610 zimepangwa kujengwa kwa kiwango cha lami na kazi ya ujenzi iko kwenye hatua ya ununuzi (kupata msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani).

Ilisema maeneo na mali zote zitakazoathirika wakati wa ujenzi katika kipande cha mita 610 kinachotarajiwa kujengwa katika mwaka huu wa fedha, zitafidiwa kabla ya ujenzi huo kuanza.

"Barabara ya Tamco kupitia Vikawe hadi Mapinga ina jumla ya urefu wa kilomita 23 ambapo kilometa 22 zimejengwa kwa kiwango cha changarawe na kilomita 1 imejengwa kwa kiwanga cha lami,"ilisema.

Ilisema barabara hiyo ni kiungo muhimu cha barabara kuu ya Morogoro na ile ya kutoka Dar es Salaam kwenda Bagamoyo kwa kuwa hutumika zaidi kukwepa msongamano wa magari kwa watumiaji wa barabara watokao Dar es Salaam na Bagamoyo bila kupita Ubungo.

Ilieleza kuwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wabarabara hiyo kwa kiwango cha lami pamoja na uhakiki wa fidia kwa maeneo na mali zitakazoathirika na ujenzi huo umekamilika.

Ilibainisha hadi sasa kilometa moja imekamilika kujengwa kutoka Kibaha kwenye eneo ambalo halihitaji kufidiwa.

# Serikali yakamilisha kazi uainishaji utalii ufukweni

WIZARA ya Maliasili na Utalii, imekamilisha kazi ya kuainisha eneo lote la fukwe za mwambao wa Bahari ya Hindi wenye urefu wa kilomita 1,423 kwa ajili ya uendelezaji wa shughuli za utalii wa ufukweni nchini.



Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na wizara hiyo ilipokuwa ikitoa majibu katika swali la Mbunge wa Mtwara Mjini (CCM), Hawa Ghasia.

Mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani kuhakikisha inatangaza utalii wa Kanda ya Kusini Mashariki, hasa fukwe za bahari za Msimbati na Mji Mkongwe wa Mikindani.

Wizara hiyo, ilisema serikali imeendelea na kazi ya kutanua wigo wa mazao ya utalii kijiografia nchini.

Ilisema serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuendeleza na kukuza mazao mapya ya utalii katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo ya fukwe za bahari na Mji Mkongwe wa Mikindani.

"Katika kuendeleza juhudi hizo, wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi ilikarabati baadhi ya majengo yanayopatikana katika Mji Mkongwe wa Mikindani na kufungua Kituo cha Mambo Kale kwa ajili ya kusimamia shughuli za uhifadhi na uendelezaji wa utalii katika eneo hilo," ilisema.

Ilisema wizara imeendelea kushirikiana na sekta binafsi pamoja na Mamlaka ya eneo la Mji Mkongwe katika kufanikisha Tamasha la Utamaduni la Mikindani linalofanyika kila mwaka.

"Tamasha hilo kwa kiasi kikubwa limeendelea kuvutia wageni na watalii kutoka ndani na nje ya nchi kutembelea Mji Mkongwe wa Mikindani na maeneo ya jirani," ilisema.




Habari na Augusta Njoji

Pia, kupitia Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) inatangaza utalii kwa ujumla ikiwamo maeneo yote ya fukwe na vivutio vya mambo ya kale kupitia njia mbalimbali za utangazaji.

Ilitaja njia hizo kuwa ni pamoja na Tovuti maalumu ya kutangaza utalii wa Tanzania (Tourism Destination Portal) na Mobile App, ambazo zinaainisha maeneo yote ya kitalii nchini Tanzania.

Ilisema kuwa kupitia njia hizo za utangazaji, maeneo ya fukwe ikiwamo yanayopatikana Kanda ya Kusini Mashariki pamoja na maeneo ya mambo kale ikiwamo Mji Mkongwe wa Mikindani yamekuwa yakitangazwa.

# Tamisemi yatenga bil. 27/- kukamilisha zahanati



OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imesema katika mwaka wa fedha 2020/21, imetenga Sh. bilioni 27.75 kwa ajili ya kukamilisha maboma 552 ya zahanati sawa na tatu kwa kila halmashauri.

Kauli hiyo ilitolewa bungeni jana na Ofisi ya Rais, Tamisemi wakati ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Maria Kangoye.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji ukamilishaji wa majengo yaliyoanzishwa na wananchi hususani zahanati.

"Je, serikali ina mpango gani wa kusaidia ukamilishaji wa majengo yaliyoanzishwa na wananchi kwa ajili ya kutoa huduma za jamii hususan huduma za afya na elimu," alihoji.

Katika majibu ya ofisi hiyo, ilisema serikali itaendelea kuunga mkono jitihada za wananchi kwa kukamilisha maboma ya miundombinu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Ilisema serikali imeendelea kuunga mkono jitihada za wananchi kwa kukamilisha maboma ya miundombinu ya afya na elimu maeneo mbalimbali nchini.

Ilifafanua kuwa katika mwaka wa fedha 2018/19, serikali ilikamilisha maboma 2,392 ya madarasa ya shule za sekondari nchini kwa gharama ya Sh. bilioni 29.9.

Katika mwaka wa fedha 2019/20 serikali imekamilisha maboma 364 ya nyumba za walimu wa shule za msingi nchini kwa gharama ya Sh. bilioni 9.1.

Ilibainisha kuwa, kwa upande wa sekta ya afya, serikali imekamilisha ujenzi wa vituo vya afya 433 ambavyo vilianza kujengwa kwa nguvu za wananchi.

ama

ALHAMISI JUNI 11, 2020

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Mzalishaji, DC wahamia vijijini kuhamasisha kwa kugawa bure**



Ukurasa 13

Ofisa TBS anyambua maana yake mtambuka, inapogeuka madhara



Ukurasa 14

**Wajane wanavyopaisha kilio katika haki inayoegemea afya**

AFYA

# Namna ulivyo unene kupindukia na madhara yake yanavyokuwa

**Na Rahma Suleiman, Zanzibar**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), kupitia miongozo yake inaitahadharisha jamii kuhusu kuwapo ongezeko la watu wenye unene wa kupitiliza, ikitaja sababu ya kuwapo watu wengi wenye maradhi ya moyo, kisukari na ini.

Kamusi ya Kiswahili Sanifu, inautafsiri unene ni hali ya mtu kujaa au kutuna mwili. Utafiti duniani, unaonyesha kwamba tatizo la unene uliopitiliza duniani huwakumba wanaume zaidi kuliko wanawake.

Mara nyingi unasababishwa na kawaida ya mtu kula chakula kingi na mwili husika unakosa mazoezi ya kutosha.

Pia, kuna visababishi mwilini pale unapokosa mazoezi yanayostahili unene unaongezeka pasipo vikwazo vya kikomo.

Urithi wa asili wa vinasaba katika familia au ukoo ambao huko nyuma ulikuwa na watu wenye maumbile hayo ya unene.

Kuna suasa la matumizi ya dawa zinazotibu baadhi ya magonjwa huzaa athari, vyote vinachangia shida ya kuongezeka uzito wa mwili.

Utafiti unaonyesha kwamba watu wanene wanaathirika zaidi na maradhi hayo, kuliko wenzao wembamba.

**UNAJIPIMAJE UZITO?**

Kupima uzito kwa jina la kitaalamu kunaitwa 'Body Mass Index au kwa kifupi BMI. Msingi wake, ni kipimo kinachotumia urefu na uzito wa mtu, kujua usahihi alikosimama kiafya, kwa kupata uwiano wake ( uzani wa mita na kilo).



Mtu mmoja katika mwonekano wa namna mbili, alipokuwa mnene na baada ya kupunguza mwili. **PICHA: MTANDAO.**

> **Kuna dawa maalumu za kukabiliana na unene, zinazotumiwa kupunguza hamu ya chakula au kuzuia ufyonzaji...**

Kwa mujibu wa WHO, inapotokea chini ya wastani 18.5, maana yake ni kwamba, kuna uzito mdogo; na ikiwa kati ya 18.5 na 24.9 unaakuwa uzito wa kawada kiafya ; kati ya 25 na 29.9 unakuwa uzito mkubwa; ilhali zaidi ya 30 unakuwa uzito mkubwa kupindukia.

**MADHARA**

Kuwa mzito mno kunaleta hatari nyingi kwa afya na kusababisha matatizo au kuongeza uwezekano wa magonjwa mengi sana .

Athari ya kwanza, ni waathirika kushuhudia ongezeko magonjwa kama vile shinikizo la damu, kisukari figo, moyo.

Unene pia unawaletea kinababa tezi dume na kinamama, wapo wanaokumbwa na tatizo uvimbe tumboni.

Pia, kwa hao wenye uzito mkubwa hupungukiwa uwezo wako wa kufikiria (IQ), baadhi wanabaki katika kiwango waalichokuwa nacho miaka 10 iliyopita.

Mnene anaelemewa na shida ya kupumua, ikiendana na matatizo ya kukoroma sana anapokuwa usingizini.

Katika orodha ndefu ya matatizo, kuna suala la mwili kuongezeka mafuta mengi na wakati huohuo, unachoka haraka.

Yapo madhara ya wanene kuwa na kawaida ya kukosa hamu ya kufanya tendo la ndoa na maumivu makali kwenye viungo, kama vile magoti na kiuno.

Mifumo yao ya kumeng'enyua chakula, nayo hukaaa vibaya na homoni za mwili zinakuwa katika mpangilio usioendana; wanaume kwa wanawake.

**MATIBABU YAKE**

Matibabu ya kupunguza uzito uliopindukia ili urudi wa kawaida huambatana, unaanzia na kuboresha mazoezi ya mwili.

Pia, kuna suala la kuimarisha ubora wa chakula mtu anavyotumia, kwa kadri inavyoshauriwa kitaalamu kwa mhusika.

Kuna dawa maalumu za kukabiliana na unene, zinazotumiwa kupunguza hamu ya chakula au kuzuia ufyonzaji mafuta mwilini.

Upande wa unene tumboni, kuna mpira mpira maalumu wa kufunga tumboni unaosaidia kupunguza uzito wa mwili.

Kuna wakati inaopibidi, kuna upasuaji maalum wa mwili hufanywa kupunguza ama ukubwa au urefu wa tumbo au vyote kwa pamoja.

Daima upasuaji huo unalenga kuujenga mwili wa mtu kushiba upesi na kupunguza uwezo wa mwili huo kufyonza virutubishi vilivyomo katika chakula.

Wataalamu wa chakula na lishe wanashauri watu wazidi kufanya mazoezi, kula vyakula kulingana na kundi lao la damu na aina ya vyakula unavyopaswa kuliwa, ili kupunguza uzito wa miili yao,

AFYA

WIKI YA MAZIWA DUNIANI

# Mzalishaji, DC wahamia vijijini kuhamasisha kwa kugawa bure



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina (wa pili kutoka kushoto), akiongoza uzinduzi wa Wiki ya Unywaji Maziwa, mjini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

**Na Renatha Msungu, Dodoma**

MAZIWA ni lishe muhimu kwa binadamu na mtoto katika nafasi ya pekee, ikibeba viinilishe muhimu na vingi kwa afya yake.

Unapotaja maziwa, kamusi ya lugha ya Kiswahili inaitafsiri kuwa "kiowevu kizito na cheupe kinachotoka kwenye titi la mnyama au binadamu wa kike.'

Katika matumizi ya kibinadamu, mbali na chanzo cha mtoto kunyonya kutoka kwa mama, pia kuna matumizi mbadala maziwa ya ng'ombe, yanayofaa kwa lishe ya jamii wa rika zote.

Kutokana na maendeleo kupiga hatua, mbali na maziwa kupatikana kwa mfumo wa kutoka vyanzo vya asili vya binadamu na wanyama, ng'ombe akizoeleka zaidi kuwa chanzo kikuu, pia yanapatikana kwa namna tofauti, yakiwamo maziwa ya unga yanayoingizwa kutoka nje ya nchi.

Inapozungumziwa kitaifa, matumizi ya maziwa ya wanyama yanasimamiwa na Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) iliyoundwa mwaka 2004, kwa jukumu la kuratibu na kuendeleza rasilimali maziwa Tanzania Bara.

Bodi inahamasisha uzalishaji, ukusanyaji na usindikaji wa maziwa, ili kuboresha masoko na unywaji wake kwa kuwawezesha wadau katika shughuli zao.

Taarifa kutoka tovuti hiyo inafafanua kwamba, kuboresha unywaji maziwa na bidhaa zake, pia soko lake kwa kushirikiana na wizara zenye dhamana na Kilimo na Mifugo, imekuwa ikiadhimisha Wiki ya Maziwa kitaifa, kuanzia mwezi Mei hadi mwanzoni mwa Juni.

> **Kwa kweli nimefurahi kuona tumeletewa maziwa, naishauri serikali iwaambie na kampuni nyingine kujitokeza kusaidia watu maziwa," anasema Lilian.**

Kimataifa, ni wiki iliyoanzishwa na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO), ikihamasisha unywaji maziwa kimataifa, kwa kuzingatia ni chakula bora kwa umma wa rika zote.

Chimbuko lake nchini, ilianzishwa na Chama cha Wafugaji wa Ng'ombe wa Maziwa wa miko ya Pwani na Dar-es-Salaam, mnamo Juni 1997, baada ya wazalishaji na wasindikaji maziwa hao kuyumba katika soko.

Taarifa za TDB zinaeleza tangu mwaka 1998, kumekuwapo maadhimisho hayo, huku kitaifa ilianzia mkoa wa Arusha mwaka 2002; Iringa, 2004; Mwanza, 2005; Tanga, 2006; Morogoro, 2007; na Mbeya, 2008.

Ilendelea Sumbawanga, Rukwa 2009; Dodoma 2010; Dar-es-Salaam 2011, Kilimanjaro, 2012; Ruvuma 2013; Mara 2014; Babati, Manyara, 2015; Njombe 2016; Kagera 2017; pia 2018 na 2019, ilikuwa mfululizo mkoani Arusha na meaka huu,

Malengo ya Wiki ya Maziwa kimsingi ni kuwaelimisha wananchi matumizi kwa rika zote na faida zake katika kujenga afya ya binadamu.

Ni tukio linalolenga kuwashawishi watunga sera umuhimu wa maziwa kiuchumi, kuwaelimisha wadau kuongeza ubora wa bidhaa za maziwa nchini na umuhimu wazalishaji kujiunga katika vyama vya ushirika

Aidha, kuna mtazamo kubadilishana ujuzi na uzoefu na baina ya wadau wa maziwa; na kuwahamasisha wadau kunywa maziwa yaliyosindikwa.

**KILICHOJIRI DODOMA**

Maadhimisho ya Wiki ya Maziwa mwaka huu Kitaifa yamefanyika Mjini Dodoma Juni 4 mgeni rasmi alikuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ambayo iliendeshwa kielektroniki.

Awali tukio hili kitaifa lilipangwa kufanyika Juni 2, lakini liliahirishwa. Kimataifa, Wiki ya Maziwa mwaka huu iliadhimshwa Juni Mosi.

Mjini hapa, pia kulikuwapo tukio la ugawaji maziwa kuuhamasisha umma kujenga mazoea ya kunywa maziwa, ni tukio lililosimamiwa na Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Patrobasi Katambi, chini ya uratibu wa wazalishaji maziwa kampuni ya Kilimanjaro, mnamo Juni Mosi.

**Huku kukiwapo misaada inayoelekezwa kwa**

vituo vya yatima, Mkuu wa Wilaya aliongoza ugawaji maziwa akianzia katika kijiji cha Matumani, chenye watoto zaidi ya 150.

Anasema, serikali imekuwa ikiwapigia kelele wafugaji wasiishie kuuza maziwa, bali na familia zao wanywe, ukiwa ndio mtazamo wa kampeni inayofanyika sasa kueneza elimu inayotakiwa, ichukue mkondo wake.

Kampuni inasema ni aina ya kampeni inayofanyika pia nje ya mkoa wa Dodoma, ikibeba sura ya kuunga mkono serikali.

Mkurugenzi wa Kilimanjaro Fresh, Irfhan Virjrr, anasema wamejijengea utaratibu wa kutoa maziwa katika maeneo wanayofanya kazi zao, ili kuhimiza unywaji maziwa kitaifa.

Anafafanua kuwa wakati Tanzania inashika nafasi ya pili ya kuwa na ng'ombe wengi barani Afrika, kuna umuhimu wa nchi kujengea utaratibu wa kunywa maziwa kwa wingi kulinda afya zao.

"Unajua maziwa ni muhimu sana kwa watoto, hivyo wazazi wanapaswa kupewa elimu ya unywaji maziwa, ili yawasaidie watoto waweze kuongeza vitamin," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema, ugawaji huo wa maziwa, hauishii katika Wiki ya Maziwa pekee, bali ni mfumo endelevu unaolenga kujenga mazoea kwa wengi kitaifa.

Inaelezwa kwamba kuwapo mwitikio mkubwa wa matumizi hayo na jijini hapa, ni hatua kubwa iliyopigwa katika imani ya matarajio mikoa mingine itafuata nyayo, pindi kampeni za waratibu zitakapowafikia.

Kwa mujibu wa waratibu hao, manufaa ya kampeni yameanza kuwafikia kupitia vyombo vya habari na matangazo mbalimbali ya ziada.

**WANYWA MAZIWA**

Mtoto Liliani Maseko, mkazi wa Mkonze, Dodoma, anakiri amefurahia kupata maziwa ya mgawo, kwa sababu yanamuongeza vitamin mwilini husisani kwa watoto wadogo.

"Kwa kweli nimefurahi kuona tumeletewa maziwa naishauri serikali iwaambie na kampuni mengine kujitokeza kusaidia watu maziwa," anasema Lilian.

Anafafanua kuwa watoto wenzake wengi wanakosa lishe sahihi kutokana na wazazi kutokujua umuhimu wa unywaji mlo huo wenye utajiri vitamini na anahimiza kampeni kama hizo kutawala.



AFYA

SIKU YA CHAKULA SALAMA DUNIANI

# Ofisa TBS anyambua maana yake mtambuka, inapogeuka madhara

- Ilivyoasisiwa na inavyomlinda mtu
- Ikikosewa; janga afya hadi uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

JUMAPILI iliyopita Tanzania iliungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha Siku ya Chakula Salama Duniani, ambayo iliridhiwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) uliofanyika Desemba 20, 2018.

Mkutano huo ulipitisha azimio lililotangaza Siku ya Chakula Salama Duniani kuadhimishwa kila Juni 7 ya mwaka na maadhimisho yamefanyika duniani kote kwa mara ya kwanza mwaka jana, 2019 yakiwa na kaulimbiu 'Chakula Salama, Jukumu la Kila Mmoja Wetu.'

Mwaka huu maadhimisho hayo yameendeleza kaulimbiu hiyo inayolenga kukumbusha, kuelimisha na kuongeza uelewa wa jamii katika masuala ya chakula salama; kutoka katika chanzo kama shambani au majini, hadi kwa mlaji.

Vilevile, maadhimisho yanatoa fursa ya kuhamasisha wadau wa chakula kujitathmini kwa wajibu wa kila mmoja kuhakikisha anakuwa na chakula salama.



Vyakula vilivyoandaliwa tayari kwa mlo. Usalama wake una mengi ya kuzingatiwa. **PICHA: MTANDAO.**

**MAANA YAKE**

Ofisa Usalama wa Chakula wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Dk. Analice Kamala, anasema 'Chakula Salama' ni kitu chochote kilichosindikwa au kisichosindikwa na kimekusudiwa kuliwa na binadamu.

Hapo anatoa mifano ya vitu vya kula kama vile vinywaji, pipi na chochote kinachotumika katika usindikaji au utayarishaji wa chakula na kisichoingia katika kundi la ama kipodozi, tumbaku au dawa.

Pia, anasema ni kile ambacho kikitayarishwa na kuliwa kama kilivyokusudiwa, hakitaleta madhara kwa mlaji.

Dk. Kamala anataja vihatarishi vya usalama wa chakula ni ambavyo kwa njia moja au nyingine vinaweza kufanya chakula kisiwe salama kwa matumizi ya binadamu. Anavieleza kugawanyika katika makundi matatu.

Mtaalamu huyo anataja kundi la kwanza kuwa ni vihatarishi cha Kibailojia (biological hazards); hapo vikijumuisha vimelea vya magonjwa kama bakteria, virusi, minyoo (parasites) na prion (protini hatari mwilini na hasa kichwani katika ubongo, kuleta madhara).

Anasema, mara nyingi hivyo huingia katika chakula kupitia malighafi zinazotumika viwandani, mazingira ambayo chakula yanaandaliwa, binadamu au wanyama.

"Hupatikana katika mazingira ambayo vyakula hivi hulimwa, kuvunwa, kuhifadhi na wakati wa usindikaji na maandalizi wakati wa kula," anasema Dk. Kamala na kuongeza:

"Wingi wa vimelea hivi hupunguzwa au kuondolewa kabisa wakati wa kupika au kusindika, pia kwa kudhibiti mfumo mzima wa uzalishaji, usindikaji na uhifadhi wa chakula (usafi, joto na muda)."

> "Hizi zinakuwapo kwa sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kutoa kinga dhidi ya uharibifu. Sumu zinazotumika kama kinga ni kama vile 'cyanide' katika muhogo, sumu kwenye samaki aina ya bunju."

Kundi la pili kwa mujibu wa Dk. Kamala, ni vihatarishi vya kikemikali vinavyopatikana ndani ya chakula au vinamuingia wakati wa uhifadhi au usindikaji.

Anasema, kemikali zimegawanyika katika makundi tofauti, zikiwamo sumu zinazopatikana ndani ya chakula husika ana anaendelea:

"Hizi zinakuwapo kwa sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kutoa kinga dhidi ya uharibifu. Sumu zinazotumika kama kinga ni kama vile 'cyanide' katika muhogo, sumu kwenye samaki aina ya bunju."

Nyingine anasema ni uchafuzi wa kemikali za sumu katika mazao ya chakula, akitao mfano katika majina yake ya sumu kuvu na madini tembo.

Eneo jingine analolitaja ni vikolezo katika chakula vinavyosaidia katika usindikaji ikiwa vitaongezwa katika kiwango kisichokubalika na mabaki ya kemikali yanayotokana na kemikali zilizotumika kwenye kilimo, mifugo au usafi wa sehemu za uzalishaji.

Anataja eneo lingine ni uchafuzi wa kemikali kwenye kitu chochote kinachogusana na chakula, akitoa mfano wa vifungashio na vifaa vya majumbani kama sufuria na sahani zinazotumika kuandaa vyakula.

Dk. Kamala anataja kundi lingine kuwa ni vihatarishi vya kimaumbo (phyisical hazards), amabavyo navyo vimegawanyika katika makundi kadhaa.

Kuna vitu vigumu vinavyosababisha majeraha na vinapatikana ndani ya chakula chenyewe, mfano vipande vya mifupa ya nyama au samaki.

Anasema uchafuzi huo unatokea wakati wa usindikaji, mfano vipande vya chuma, glasi ambayo mionzi inayotumika katika kuhifadhi chakula inapoingia kwenye chakula kwa bahati mbaya.

**MADHARA AFYA**

Ofisa Usalama wa Chakula wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Dk. Analice Kamala, anafafanua kwamba maadhimisho hayo yana umuhimu mkubwa kitaifa na kimataifa, kwani usalama wa chakula ni kitu kisichoepukika.

Ofisa huyo anataja athari za chakula kisicho salama ni pamoja na za kiafya, akieleza zipo zinazojitokeza ndani ya muda mfupi, mfano kuumwa tumbo, kutapika, kuhara na kuhara damu.

Dk. Kamala anataja zingine za muda mrefu, akitoa mfano maradhi ya kansa, upungufu wa kinga mwilini na udumavu kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Mtaalamu huyo anasema kila mtu yuko kwenye hatari ya madhara hayo kiafya na anataja makundi maalum ya wagonjwa, wajawazito, watoto na wazee walio hatarini zaidi kuathirika na chakula kisicho salama.

**ATHARI KIUCHUMI**

Kwa upande wa kiuchumi, Dk. Kamala anasema katika biashara za ndani, za kikanda na za kimataifa, chakula kisichokuwa salama husababisha athari mbalimbali.

Anataja athari hizo kuwa ni pamoja na kukataliwa kwa bidhaa za chakula zilizozidi viwango vinavyokubalika katika soko, inakosesha mapato.

Eneo lingine analitaja ni kupungua akiba ya chakula, kwa maana anayoifafanua kitalamau kwamba chakula kilichochafuliwa zaidi ya kiwango kinachoruhusiwa, huwa hakifai kwa matumizi ya binadamu na kinapaswa kuharibiwa.

Athari nyingine anaitaja ni kuongezeka gharama za matibabu na kupungua nguvu kazi katika uzalishajimali, kutokana na watu wengi kuwa wanaugua ua kuuguliwa na ndugu wa karibu kutumia muda mrefu na gharama kubwa kuwahudumia.

**NAMNA KUNUSURU**

Ili kuwa na chakula salama, Dk. Kamala ana ushauri kwamba kunatakiwa kuwapo mfumo thabiti wa usimamizi na udhibiti wa uzalishaji, usindikaji, usambazaji na uhifadhi wa chakula ama kilichopo au kinachohitajika.

Anasema lengo kuu ni kuwa na mfumo imara wa chakula salama na kujenga mazingira yatakayotoa uhakika wa uzalishaji chakula, ambacho ni salama kwa ajili ya kulinda afya ya mlaji na kukuza biashara yao.

Dk. Kamala,anataja misingi imara ya usimamizi wa usalama inahusisha: Uwepo wa sheria; muundo wa kitaasisi kwa maana ya usimamizi; mfumo wa ukaguzi na ufuatiliaji; huduma za maabara na elimu kwa umma.

AFYA

# Wajane wanavyopaisha kilio katika haki inayoegemea afya

## • Mwenyekiti: Bado pagumu, safari ndefu

**Na Sabato Kasika**

UNAPOFANYIKA uchambuzi wa uwiano wa haki kijamii, wajane wako katika wanaoumia zaidi. Ni kundi linalokumbana na changamoto lukuki zikiwamo tabia ya miaka nenda rudi ya kuwapora mali, hata matukio ya kudhalilisha nafsi zao.

Katika moja ya maadhimsho ya siku yao jijini Dodoma, walisema katika madhila yanayowakumba, ujane huwafanya wasononeke na sasa wanaiomba serikali kuandaa Sera ya Taifa itakayotambua kuwa kundi maalum katika jami, ili haki zao zilindwe.

Mtazamo mahsusi uliopo ni kwamba, inapoanzishwa sera inayowasaidia kutoa msukumo wa jamii kuhusu haki dhidi ya madhila wanayowafikia.

Mkurugenzi wa Chama cha Wajane Tanzania (Tawia), Rose Sarwat, anasema wanahitaji upendo wa kifamilia na jamii na kutiwa moyo kwa ujumla, lakini kuna mbadala anaoufafanua kuwa: "Wanapofiwa hujikuta katika changamoto hizo ambazo mwisho wa siku zinawakatisha tamaa na kujiona hawana umuhimu katika jamii."

Rose anasema kuwapo manyanyaso huwaathiri kisaikolojia na kuna wakati inawapotezea maisha wahusika ndani ya muda mfupi, baada ya kufikwa na umauti wa wenza zao, sababu kuu ni msongo wa mawazo.

"Tatizo kubwa la kukosa uhakika wa matibabu wanapougua kwa sababu ya uduni wa maisha yao, sisi kama chama tumejitahidi ili kila mmoja awe na Bima ya Afya, lakini tumekwama," anasema Rose.

Anafafanua kwamba walipata maelekezo kutoka kwa viongozi wa mamlaka za Bima ya Afya kitaifa, lakini ilishindikana na wakashauriwa wasubiri utaratibu wa kitaifa wa bima kwa wote.

"Wajane wana changamoto nyingi, lakini hii ya ukosefu wa Bima ya Afya inahitaji kutatuliwa mapema kutokana na umuhimu wake, ili wanachama wetu waondokane nayo," anasema.

**KWANINI BIMA AFYA?**

Rose anasema, Bima ya Afya ni umuhimu na inapunguza gharama za matibabu, kutokana na ukweli uliopo kwamba, huduma ya afya ni kipaumbele cha kila mwanadamu.

Anasema, chama kimekuwa kikihangaika kuwatafutia wanachama Bima ya Afya, lakini hakijafanikiwa, ingawaje katika upande wa pili wa shilingi, hawajakata tamaa kufuatilia kulingana na maelekezo waliopewa.

"Afya bora huwapa watu utu na matumaini, hivyo kupata huduma bila changamoto ni jambo muhimu kwa watu wote wakiwamo wajane ambao wengi wao wanaishi maisha ya kawaida," anasema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Tawia, Rose Sarwatt (katikati mwenye nguo nyekundu) akiwa na wajane kwenye moja ya maadhimisho ya Siku ya Wajane Duniani. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

> **"Tatizo kubwa la kukosa uhakika wa matibabu wanapougua kwa sababu ya uduni wa maisha yao, sisi kama chama tumejitahidi ili kila mmoja awe na Bima ya Afya, lakini tumekwama," anasema Rose.**




Mkurugenzi Mtendaji wa Tawia, Rose Sarwatt akihojiwa na vyombo vya habari

**WAAMUA KUJIHUDUMIA**

Rose anasema wakati wanasubiri utaratibu wa kiserikali kupata Bima ya Afya, wanaendelea kuwahudumia kwa njia mbalimbali wanachama wao wasio na uwezo, japo anafafanua si za uhakika zaidi kimatibabu.

Mkurugenzi huyo anataja njia mojawapo ni ya kuwatambulisha wajane kwenye uongozi wa serikali za mtaa na wanapewa barua maalumu za kwenda nazo hospitalini wanapoumwa, huko wanapatiwa huduma za afya.

Hata hivyo anakiri, njia hiyo bado ina changamoto na ndiyo maana wanahangaikia Bima ya Afya.

Pia, anataja kuwapo mbadala wajane wenye umri wa miaka 60 na zaidi wanawapigania kuingizwa katika kundi la wazee wanaopata huduma za afya bure.

"Wengi ni wale wenye uwezo mdogo kimaisha, kwa maana hiyo hawana uwezo kiuchumi. Wanatakiwa kusaidiwa kupata huduma afya kadri inavyowezekana," anasema.

Rose anafafanua kwamba, inapotokea mjane anugua na kukosa matibabu, athari ya moja kwa moja kwa familia inajitokeza kwa kukosa mahitaji, kwa vile mtafutaji riziki ya kundi hilo anakuwa kitandani.

Ili mambo yawe sawa na yaende, ni matibabu yanayomuwezesha kurejea afya yake ya awali na kuendelea na shughuli za kutafuta riziki. Bima ya Afya, anayolilia ndio msingi wanaolilia.

**KILIPOTOKEA CHAMA**

Ni chama kilichoanzishwa mwaka 2014, kwa lengo la kuwaweka wajane pamoja, ili watambuane, kufahamianana na kuzijua changamoto mbalimbali za pamoja wanazopitia kisha zikapatiwa ufumbuzi.

Vilevile, ni chama ambacho kwa kushirikiana na taasisi nyinginezo wadau, pia mamlaka za kiserikali, kinajihusisha na utoaji elimu kwa jamii imayomhusu mjane, kuwapenda, kuwathamini na kuwasaidia kwa namna mbalimbali.

Ni hatua inayolenga kujitoa kwa hali na mali kumsaidia kupambana na changamoto anazopitia mjane, kusimamia sheria inayomtetea mjane huyo wa Kitanzania, ikiwamo hati ya mirathi na usimamizi wa mali za familia baada ya kifo cha mume wake.

"Chama kinalenga kurejesha matumaini mapya kwa mjane na wajane watarajiwa, huku kikijihusisha na haki za mgane na watoto walioachwa na wazazi," anasema.

Mtazamo wa Tawia ni kuhakikisha yatima wanaendelezwa kimasomo kadri inavyowezekana, pia wajane wanapatiwa elimu sahihi inayojitosheleza ya sheria, afya, saikolojia, biashara na ujasiriamali.

**CHANGAMOTO**

Mkurugenzi huyo anataja changamoto zinazowakabili, kwamba unapotokea msiba wa mume ukiwa ni wakati unaohitaji upendo zaidi kutoka kwa jamii, kinyume chake wajane wamekuwa wakitengwa, wanayanyaswa na ndugu, jamaa na marafiki wa karibu zaidi.

Analalamika mjane kuonewa na kuumizwa katika jamii na kwamba wengi wamenyanyasika kijinsia na kuathiriwa kisaikolojia, hata wengine kupoteza maisha, muda mfupi baada ya kufiwa na waume zao.

Rose anasema, kuna wajane waliumia kisaikolojia na walijikuta wanaingia katika uamuzi wa hatari kimaisha, wakidhani wanapoteza maisha, hivyo hatari na janga la msiba linafika hatua mbaya zaidi.

"Mjane anahitaji kuwa na afya njema kuanzia kiakili na kimwili. Hivyo wasaidiwe kwa kila hali, kuondokana na hayo, ili waweze kujenga kikamilifu familia walizoachiwa na wenzi wao," anasema.





# Wamilikishwa maeneo baada ya mgogoro

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANANCHI wa eneo la Mbuyuni Kizota jijini Dodoma, wameanza kumilikishwa maeneo yao baada ya kumalizika kwa mgogoro uliodumu kwa miaka 30.

Awali, eneo hilo lilikuwa na mgogoro juu ya uhalali wa makazi ya wananchi wa eneo hilo, huku likiwa limepangiwa matumizi mengine na wananchi kutakiwa kuvunja nyumba zao.

Akizungumza na wananchi wakati wa uwekaji wa alama ya mpaka (beacon) kwa kaya zaidi ya 8,100, Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alisema wananchi hao waliishi kama ndege wa mwituni ambao walikuwa hawajui pakuishi kutokana na kutohalalishiwa makazi yao.

"Mmeishi maisha magumu mlikuwa hamjui kesho yenu leo tumeandika historia upya, hamkulala usingizi, leo Mbuyuni mtapata amani kazi hii ifanyike," alisema.

Mavunde ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, alisema hawezi kufanya siasa kwenye maisha ya watu kwa kuwa dhamira yake ni kuona wananchi wana amani.

"Kazi yetu ni kuwaletea maendeleo nawaomba Oktoba msikosee kama ilivyo ada mafiga matatu yatimie," alisema.

Alimshukuru Mkurugenzi wa Jiji hilo, Godwin Kunambi, kwa kufanikisha zoezi hilo kwa kuwa awali majibu ya iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA) yalikuwa yanakatisha tamaa.

Naye, Mwenyekiti wa makazi eneo hilo, Hemed Mdima, alimshukuru Rais John Magufuli na Mbunge huyo kwa kuwezesha eneo hilo kupimwa na sasa ni wakazi rasmi wa eneo hilo.

**Mmeishi maisha magumu mlikuwa hamjui kesho yenu leo tumeandika historia upya, hamkulala usingizi, leo Mbuyuni mtapata amani kazi hii ifanyike**

# Serikali yaiagiza TBL kuhusu kiwanda

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeuagiza uongozi wa kiwanda cha bia Tanzania (TBL) kufungua au kukikodisha kiwanda cha Kilimanjaro ambacho kipo mikononi mwao ili kianze kazi mara moja.

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, katika mkutano wake na wanunuzi wa mazao ya zabibu na shahiri pamoja na wakulima wa mazao hayo.

Alisema kuwa kwa sasa wakulima wa shahiri hawana soko, hivyo ni vyema kwa msimu ujao wakulima walime zao la shahiri.

"Tunataka kiwanda kianze kazi mara moja, lengo ni kutaka wakulima kulima kwa msimu ujao na sisi serikali tutahakikisha mikataba inakuwa sawa kwa pande zote mbili kwa mnunuzi na mkulima na uwazi wa mikataba hiyo ili kila mmoja kunufaika katika zao hilo," alisema.

Alisema serikali imekutana na wadau wa mazao hayo, ili kutatua kero zilizopo katika sekta ndogo ya zabibu ili kukuza soko la mazao hayo na kuinua kipato cha wakulima wake.

Aliwataka wakuu wa wilaya, wakuu wa mkoa na warajis wa vyama vya ushirika watakaposaini mikataba hiyo na serikali ishirikishwe kikamilifu ili kulinda maslahi ya mkulima na wanunuzi.

Kuhusu zao la zabibu, Bashe alisema msimu wa kilimo unaanza mwezi wa nane, hivyo serikali inahitaji uhakika wa masoko na wanunuzi wanatakiwa kusema namna ambavyo watanunua zao hilo.

"Hatutaki wakulima wa zabibu mwezi wa nane wakati wa kuvuna wapate shida ya masoko na nahitaji kujua kwa mwezi huo tutavuna kiasi gani. Njia pekee itakayotusaidia ni kuingia mkataba na wakulima," alisema.

Alitoa kwa wakulima kutotegemea zao moja bali wajikite pia kwenye mazao mengine na kuwataka kampuni ya wanunuzi kununua shahiri kwa wakulima wote.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Theresia Mahongo, alisema zao la shahiri ni la kibiashara linalowaingizia uchumi wakulima.

Alitoa rai kwa wanunuzi kuongeza tani kwa zao la shahiri kwani wakulima wanalima zaidi ya tani 8,000 zinazohitajika.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa TBL, Philip Redman, alisema kwa msimu ujao wa 2021, wameingia mkataba na wakulima 300 na kiwanda kina uwezo wa kuchukua tani 5,000 kwa mwaka.

Kwa upande wa Kiwanda cha Bia cha Serengeti (SBL), Mkurugenzi wake wa uhusiano, John Wanyancha, alisema kwa msimu ujao wanatarajia kuchukua tani 3,000 kwa wakulima 60.

Mmoja wa wakulima wa shahiri, Domisiani William, alisema tatizo wanalokumbana nalo ni bei ndogo ya na kuomba serikali kuongeza tani kwani wakulima wanalima zaidi.



Rundo la takataka likiwa limetelekezwa bila ya kuzolewa katika eneo la stendi ya daladala ya Sabasaba, jijini Dodoma jana, kitendo kinachohatarisha usalama wa afya za watu na kinaweza kusababisha magonjwa ya milipuko. **PICHA: PETER MKWAVILA** .

# Waziri aridhishwa ujenzi wa hospitali

**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameonyesha kuridhishwa na kasi ya ujenzi unaoendelea katika Hospitali ya Uhuru iliyopo Wilaya ya Chamwino.

Akizungumza baada ya kutembelea eneo la ujenzi wa hospitali hiyo, Jafo alisema ujenzi unaridhisha na kwamba kazi iliyobaki ni ndogo ikilinganishwa na awali ilivyokuwa.

Alisema awali ujenzi ulisuasua kutokana na mvua na kwamba kwasasa kasi iliyopo ni nzuri na litakamilika kwa wakati.

"Naona hapa kazi kubwa imefanyika, na nimeridhika na hapa tulipofikia, jana (juzi) nilikuwa Kigamboni kukagua ujenzi wa nyumba na siku nne zilizopita nilikuwa Uvinza ambapo huko wenzenu niliwakoromea kwa sababu walinipa kichefuchefu," alisema.

Aliagiza kurekebishwa kwa upungufu wowote kwenye ujenzi huo na Mkandarasi wa Suma JKT kwa kushirikiana na Mshauri Mwelekezi wa Wakala wa Majengo (TBA), washauriane kuangalia namna ya kuongeza ghorofa moja.

"TBA leo Jumatano nitakuja Jumanne ya wiki ijayo ili tupate majibu ya makubaliano mliyoafikiana nyie, kama waweke zege kuruhusu kujengwa kwa ghorofa moja juu hapo baadaye au muezeke," alisema.

Akizungumzia katika ziara yake ya siku saba katika mikoa 12, Waziri Jafo alisema kazi zinazofanyika za ujenzi zinaendelea vizuri na kudai kuwa ujenzi wa hospitali hiyo unaenda vizuri licha ya changamoto za awali.

"Natamani mradi wa Kigamboni ungefanywa na Suma JKT kwa sababu wametekeleza mradi wa Hospitali ya Uhuru vizuri kwa uaminifu," alisema.

Jafo pia aliuagiza uongozi wa Suma-JKT ambaye ndiye mkandarasi wa ujenzi wa hospitali hiyo kuhakikisha wanasimamia kikamilifu ili kukamilisha kazi hiyo kwa wakati uliopangwa.

Naye, Mhandisi kutoka Suma JKT, Omary Kabalagu, alisema wanatarajia kukamilisha ujenzi huo Agosti mwaka huu, ambapo awali walitakiwa kukamilisha Mei 25, mwaka huu.

Alisema ujenzi ulisuasua kutokana na mvua nyingi zilizonyesha mwaka huu.

Kwa upande wake, Meneja wa TBA Dodoma, Victor Batazary, alisema hali ya ujenzi inaendelea vizuri na hawajapata mashaka yeyote.

Hospitali ya Uhuru inajengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 3.99, fedha zilizotolewa na Rais Magufuli baada ya kuahirisha Sherehe za maadhimisho ya Siku ya Uhuru, Desemba, 9 mwaka 2018 na zile zilizotokana na gawio la kampuni ya Airtel.

HABARI MBEYA

# Magufuli aamuru Tanroads kurudishia wananchi ardhi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

RAIS John Magufuli ameamuru Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) kuachana na mpango wake wa kutwaa eneo la wananchi katika Kijiji cha Isyonje wilayani Rungwe kwa ajili ya kujenga mizani ya kupima uzito wa magari kwenye Barabara Kuu ya Tanzania na Malawi.

Rais Magufuli alitoa agizo hilo juzi wakati alipopigiwa simu na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila na kuzungumza moja kwa moja na wananchi wa Kijiji cha Isyoje waliokuwa wamekusanyika kwenye mkutano wa hadhara.

Akizungumza na wananchi hao kwa njia ya simu akiwa Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma, Rais Magufuli, alisema amesikia kilio chao baada ya kuona kwenye televisheni wakilalamika kuhusu Tanroads kuchukua ardhi yao bila kuwalipa fidia.

Alisema Sheria ya Ardhi namba tatu na namba nne ya mwaka 1999 inaamuru kulipa fidia kabla ya kuchukua ardhi ya wananchi, lakini Tanroads hawakuizingatia na badala yake walichukua ardhi ya wananchi kwa zaidi ya miaka mitatu sasa bila kulipa fidia jambo ambalo hilo ni kinyume cha sheria.

"Naamuru Tanroads kuachana na eneo hilo na badala yake wananchi waendelee na shughuli zao za kiuchumi, kama ni nyumba wajenge na kama ni mizani itajengwa sehemu nyingine sio hapo," alisema Rais Magufuli.

Rais Magufuli aliwaomba radhi wananchi hao kwa watendaji wake kuwacheleweshea maendeleo kutokana na kitendo hicho cha kuwazuia kuendeleza maeneo yao bila kuwalipa fidia kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema Rais Magufuli anawapenda na hapendi wananchi wanyonge waonewe, na ndio sababu baada ya kusikia kilio chao alimpigia simu na kumwamuru afike kijijini hapo kuwarejeshea eneo lao ambalo lilikuwa limechukuliwa na Tanroads.

Alisema kuwa baada ya uamuzi wa Rais, hakuna mtu yeyote atawasumbua tena hivyo akawataka waendelee na shughuli zao bila wasiwasi.




Meneja Mkuu wa Kampuni ya Cherry Garments and Safety Solutions Ltd, Dennis Kwame Simba (kushoto), akikabidhi msaada wa barakoa kwa Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi, jijini Dar es Salaam juzi, kwa ajili ya watoa huduma na wagonjwa waliolazwa hospitalini hapo. Wa tatu kushoto ni Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Selina Koka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Machinga kupewa vitambulisho 3,500

**Na Grace Mwakalinga,** ILEJE

VITAMBULISHO 3,500 vinatarajiwa kugawiwa kwa wajasiriamali wadogo wilayani Ileje mkoani Songwe kwa lengo la kuwawezesha kufanya kazi zao kwa utulivu kama akivyoagiza Rais John Magufuli.

Akizungumza wakati wa kikao kazi kilichowahusisha watumishi Mkuu wa Wilaya hiyo, Joseph Mkude, alisema mwaka huu wamepokea vitambulisho vichache ukilinganisha na mwaka jana ambapo walipokea 5,600.

Alisema kwa mujibu wa sensa waliyoifanya mwaka huu, walibaini idadi ndogo ya wajasiriamali ukilinganisha na mwaka jana kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kuhama, vifo pamoja na janga la corona ambalo limechangia mitaji yao kufa.

Aidha, aliwasisitiza wajasiriamali kutumia vyema fursa waliyopewa na Rais ya kupata vitambulisho ili waendelee kufanya shughuli zao bila usumbufu kutoka kwa wakusanya kodi au ushuru.

"Nawaomba wasimamizi wa zoezi hilo, wataalamu kutoka ofisi yangu pamoja na watendaji wa kata kuhakikisha mnalisimamia kulingana na maelekezo ya serikali pasipo kuwanyanyasa wajasiriamali kwa kuendekeza undugu au kabila lolote mwenye sifa lazima apewe," alisema Mkude.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Haji Mnasi, aliahidi kusimamia vyema zoezi hilo kwa kuhakikisha wajasiriamali wote 3,500 ambalo walisajiliwa wanapatiwa vitambulisho.

Alisema ugawaji vitambulisho unafanyika kidijitali, na kwamba watendaji wote wa kata 18 za wilaya hiyo waligawiwa kulingana na takwimu za wajasiriamali kwa eneo husika.

Utaratibu wa kugawa vitambulisho vya wajasiriamali nchini ulianza mwaka 2019, baada ya Rais Magufuli kubaini kero mbalimbali zilizokuwa zinawakabili kwenye mazingira ya shughuli zao, na kwamba lengo lake ilikuwa ni kuwalinda na kuongeza mapato ya serikali.

# Vijana wachangia damu hospitali ya wazazi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VIJANA 20 wa kikundi cha Power Group kilichopo Kata ya Iyela jijini Mbeya, wamejitokeza kuchangia damu katika benki ya damu salama iliyopo kwenye Hospitali ya Wazazi Meta mkoani Mbeya, kwa lengo la kuokoa maisha ya wajawazito, mtoto na waathirika wa ajali.

Wakizungumza jana baada ya kuchangia damu, baadhi ya vijana hao walisema kuna upungufu mkubwa wa damu salama kwenye vituo vya kutolea huduma, ambapo baadhi ya kinamama na watoto hupoteza maisha kwa kukosa damu.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Power Group, Samwel Mambosasa, alisema walitembelea hospitali hiyo na kubaini kuwa kunauhitaji mkubwa wa damu na ndipo walipoamua kujitolea kutoa damu ili kukabiliana na changamoto hiyo.

"Tunapoelekea kwenye kilele cha maadhimisho ya uchangiaji damu nchini tuhakikishe tunamaliza kabisa tatizo la uhaba wa damu hospitalini ili kunusuru maisha na wenzetu ambao wanapata ajali au kinamama wanapojifungua kwa kutambua umuhimu huo kikundi chetu kiliamua kujitoa," alisema Mambosasa.

Alisema wamechangia zaidi ya chupa 20 za damu na kwamba zoezi hilo litakuwa endelevu kwao na kwamba wataendelea kuhamasisha na kupeana elimu juu ya umuhimu wa kuchangia damu.

Miongoni mwa wanakikundi hao, Jeska Moses, alisema moja ya makundi ambayo yako hatarini ni la wajawazito, na kuwa wanapojifungua hupoteza damu nyingi, hivyo uchangiaji wa damu kwa hiari unaweza kuokoa maisha yao.

Aliwaasa kinamama wengine kujenga utamaduni wa kuwachangia wenzao, ambao wanajifungua na kusisitiza kuacha tabia ya kujifungulia nyumbani kwa kuwa wanaweza kupoteza maisha bila kupata msaada wa wataalamu wa afya.

Ofisa Ustawi wa Jamii Benki ya Damu Salama Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Latifa Nyankunga, alisema kuna uhitaji mkubwa wa damu katika hospitali na vituo vya afya vilivyopo Nyanda za Juu Kusini, hivyo aliwataka watu wengi zaidi kujitokeza kuchangia damu.

"Idadi ya vituo vya afya imeongezeka sana kwenye kanda yetu ya Nyanda za Juu Kusini, lakini hata hospitali zetu kongwe pamoja na vituo vipya vya afya vinakabiliwa na upungufu mkubwa wa damu… hivyo tunaomba watu wengi wajitokeze kuchangia damu ili tuweze kukidhi mahitaji ya vituo vyetu vya afya," alisema Nyankunga.

Hospitali ya Wazazi ya Rufani Meta, ndiyo inayoongoza kwa kuwa na mahitaji makubwa ya damu kutokana na kuhudumia kinamama wengi wanaokwenda kujifungua pamoja na watoto wachanga.

# ‘Uhakiki wapigakura ishara kuimarika kidemokrasia’

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed, amesema kurejea kwa uandikishaji na uhakiki wa taarifa za wapigakura kwa mikoa yote ya Zanzibar ni ishara ya mafanikio kwa nchi yenye nia ya kuimarisha demokrasia nchini.

Akizungumza katika kituo cha uandikishaji cha Bungi, wakati akifanya ziara kwenye vituo hivyo, alisema hatua hiyo imewajengea imani wananchi na kuondoa malalamiko ambayo yangeweza kujitokeza katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu.

Ayoub alisema kuwa ni jukumu la viongozi wa vyama vya siasa kuhakikisha wanaendesha siasa za kistaarabu na kufuata sheria, kanuni, miongozo na taratibu zinazotolewa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), ili kufikia dhamira ya kuendesha uchaguzi mkuu na kuufanya kuwa huru na wa haki.

Alisema viongozi wa mikoa na wilaya wanajukumu la kuwahamasisha wananchi ili wajitokeze kujiandisha na kuhakikisha hali ya utulivu na amani inakuwapo katika maeneo ya vituo vya kujiandikisha.

“Sisi viongozi wa mikoa na wilaya tunajukumu la kuwahamasisha wananchi waendelee kujitokeza kujiandikisha...” alisema.

Mawakala wa vyama mbalimbali vya siasa katika vituo vya uandikishaji walitoa ushauri kwa ZEC kuendelea kutoa mafunzo kwa wapigakura licha ya mafanikio yanayopatikana hivi sasa katika vituo vya uandikishaji na uhakiki wa taarifa za wapigakura ili wananchi waendelee kujitokeza zaidi.

Kazi ya uandikishaji na uhakiki wa taarifa za wapigakura imekamilika kwa mikoa yote ya Pemba na Mkoa wa Kaskazini na Kusini Unguja, kwa upande wa Unguja ambapo kazi hiyo iliendelea kwa siku mbili Juni 9 na 10 Wilaya ya Magharibi ‘A’ na Wilaya ya Magharibi ‘B’ na kukamilisha mzunguko wa ratiba ya uandikishaji katika Wilaya ya Mjini Juni 11 na 12.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe (kulia), akiteta jambo na Mwakilishi wa Kuteuliwa na Rais, Ahmada Yahya Abdulwakil, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA|: RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR**

# Rais Shein asifu Mapinduzi kuleta haki sawa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema mafanikio ya utekelezaji wa haki za binadamu na utawala bora Zanzibar yanatokana na utekelezaji wa azma ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964.

Hayo aliyasema Ikulu Zanzibar, wakati alipofanya mazungumzo na ujumbe wa uongozi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ukiongozwa na Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji mstaafu Mathew Pauwa Muhina Mwaimu, wakati ujumbe huo ulipokwenda kujitambulisha.

Rais Dk. Shein alisema, Mapinduzi matukufu ya Januari 12, 1964 yalikuwa na azma ya kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapata haki zao za msingi ikiwamo elimu, afya bure na ardhi, mambo ambayo kabla ya Mapinduzi yalitolewa kwa ubaguzi.

Dk. Shein alisema Zanzibar ina historia kubwa ya kupambana na juhudi za kuhakikisha wananchi wake wanapata haki zao za msingi pamoja na kuwapo kwa utawala bora tangu kupatikana kwa uhuru wa Zanzibar.

Dk. Shein alisema, hatua hizo zimeifanya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuendeleza haki za binadamu na utawala bora na kuipaisha Zanzibar kidemokrasia.

Alisisitiza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haiko tayari kukiuka vifungu vya Katiba na sheria zilizopo katika suala la haki za binadamu na utawala bora na badala yake itaendelea kufuata taratibu zilizopo kwa ajili ya manufaa ya nchi na wananchi wake.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepata mafanikio makubwa katika sekta za elimu na afya kutokana na kutekeleza vyema lengo na azma ya Mapinduzi ya wananchi kupata haki zao za msingi ambazo hapo mwanzo hawakuzipata.

Kadhalika, alisema hatua hiyo ndiyo iliyoifanya Serikali ya Awamu ya Saba baada ya kuingia madarakani chini ya uongozi wake baada ya uchumi kuimarika kuendeleza azma ya Mapinduzi ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma muhimu bila ya malipo ikiwamo afya na elimu.

Aliipongeza Tume hiyo kwa kufanya kazi zake vyema na kusisitiza kuwa serikali itaendelea kushirikiana nayo ili iweze kufikia malengo iliyoyakusudia.

Alisema Zanzibar haina utamaduni wa kuvunja haki za binadamu na badala yake imekuwa ni nchi yenye kufuata na kutekeleza haki za binadamu, utawala bora na demokrasia kwa vitendo.

Kwa upande wa mafanikio yaliopatikana nchini katika kupambana na janga la Covid-19, Dk. Shein alisema Jamhuri ya Muungano ikiwamo Zanzibar imepata mafanikio makubwa kutokana na mikakati maalum iliyoiweka hali iliyosaidia kupungua kwa janga hilo kwa kiasi kikubwa.

Alisema serikali zote mbili zitaendelea na mikakati hiyo iliyoiweka ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya janga hilo kwa wananchi wake bila ya kuiga wala kufuata taratibu na mipango ya wengine na badala yake itafuata taratibu ilizoziweka bila ya kushurutishwa.

Naye Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Jaji mstaafu Mwaimu, alisema Rais Shein katika uongozi wake amefanya mambo mengi mazuri kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar ukiwamo utekelezaji wa haki za binadamu na utawala bora kwa vitendo.

Alisema hali ya kisiasa imeendelea kuwa shwari zaidi na jitihada za Rais Dk. Shein zimeonekana dhahiri katika kulinda na kukuza haki za binadamu kama zilivyoorodheshwa katika Katiba ya Zanzibar hasa haki za kijamii.

Alisema wameshuhudia kuwapo kwa shule nyingi na vituo kadhaa vya afya ambavyo vingine vinaendelea kujengwa hali inayoonyesha serikali imetilia mkazo kuendeleza haki ya afya na wananchi kupata elimu bora.

Pia, alisema ana matumaini makubwa kuwa uchaguzi mkuu ujao utakuwa wa amani.

Alisema Tume hiyo inafurahia na kuunga mkono uwapo wa haki za binadamu katika Katiba ya Zanzibar na haki zilizopo katika Katiba na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mikataba mbalimbali ya kimataifa.

# Tamwa yapongezwa kuwezesha wanawake kiuchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAVIKUNDI vya ujasiriamali Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba, wamekishukuru Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa) Zanzibar kwa juhudi za kuwawezesha kujiinua kiuchumi kupitia vikundi hivyo.

Wakizungumza na Nipashe, walisema kupitia vikundi hivyo vinavyosimamiwa na Tamwa Zanzibar, kupitia mradi wa kuwawezesha wanawake kiuchumi, vimewasaidia kuongeza ushirikiano katika shughuli za uzalishaji na kuongeza hamasa kwa wanawake wengine katika jamii.

Bijuma Hamis Kombo, mwanachama wa kikundi cha Safinia, kilichopo Shehia ya Majenzi Micheweni, alisema vikundi hivyo ni mkombozi kwa wanawake wengi kutokana wengi wao huvitumia kama sehemu ya kujikwamua kiuchumi.

“Vikundi hivi vimetusaidia kupata sehemu ya kujikwamua kiuchumi kwani kupitia hisa tunazoziweka, mwanachama anaweza kukopa kwenye kikundi na kuendeleza shughuli zake mwenyewe,” alisema Bijuma.

Alisema kupitia vikundi hivyo vimemsaidia kuongeza kipato kwa familia yake kupitia mikopo hiyo.

“Mwanzo kabisa nilikopa Shilingi laki moja, nikapasisha leseni ya pikipiki yangu (bodaboda) ili kupata pesa za kuweka hisa na nashukuru Mungu naendelea na biashara yangu na hisa naendelea kuweka bila shida yoyote,” alisema.

Naye Asha Moh’d Said kwa upande wake alisema kupitia vikundi hivyo vimemwezesha kuongeza mtaji wa shughuli zake za ufumaji na ushonaji na kuongeza soko lake zaidi.

“Mimi nilikopa shilingi laki tatu kwenye kikundi changu nikaongezea mtaji wa biashara ya vitambaa na mashuka. Tunashukuru sana vikundi vimetusaidia sisi wanawake kukwamuana sisi kwa sisi,” alisema Asha.

Kwa upande wake Ramla Suleiman Khamis, kutoka kikundi cha Tuko Pamoja, amesema licha ya mafanikio hayo, vikundi hivyo vinakabiliwa na tatizo la ukosefu wa soko la uhakika wa bidhaa zao jambo linalochelewesha kasi ya maendeleo yao.

“Tunashukuru sana Tamwa Zanzibar wametusaidia, sasa umaskini unapungua taratibu kwetu, lakini changamoto yetu kubwa ni masoko. Tunazalisha sabuni, mafuta na kushona mashuka, lakini sehemu ya kuuza ni kikwazo kikubwa jambo linalosababisha wengine kutaka tamaa,” alisema.

Aliomba kupatiwa msaada wa utafutaji wa masoko ili kuwawezesha bidhaa zao kuuzika na kuendelea kuzalisha kwa wingi kwa lengo la kuwainua wanawake kiuchumi.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI YA DEREVA NA MAUZO** Mwenye uzoefu wa kuuza Maji. PIga simu namba : **0767 269677 saa za kazi**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**MIRIAM BETHUEL PETRO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0409.0031.2013** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MORINGE SOKOINE SEKONDARI mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/440356/2020.**

**MHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;113/2020**

**Ombi la RAJABU NASSORO KANYALA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu NASSORO KANYALA MAGANGA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 22/06/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 07/05/2020.

115771002

## KUPOTEA KWA HATI YA KIWANJA

**DIONIZI MWANDU MAHIZI** MKAZI WA IBINZAMATA MANISPAA YA **SHINYANGA.** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA KIWANJA **NAMBA 79 KITALU "Z"** IBINZAMATA MANISPAA YA SHINYANGA AMBAYO ILIPOTEA MWAKA 2006 MAENEO YA IBINZAMATA SHINYANGA. KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA DIONIZI MWANDU MAHIZI KWA **SIMU NAMBA 0752146056 AU 0710146050**
**RB NAMBA SHY/RB/ 3399/ 2006.**

115770102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HATI YA KIAPO**

Mimi **TUNUTU NASSORO CHAPA,** 53 umri, mdigo, wa S.L.P Tanga, nikiwa mtu mzima na akili zangu timamu naapa na kuthibitisha mbele ya Hakimu Mahakamani kama ifuatavyo;

1. Kwamba mimi **TUNUTU NASSORO CHAPA** ni mkazi wa Kata ya Duga Mtaa wa Mabawa Jiji la Tanga.
2. Kwamba **TUNUTU NASSORO CHAPA** ni msimamizi wa mirathi ya marehemu **HATIBU JUMA HATIBU** No. 25/2020 katika Mahakama ya Mwanzo Mjini Tanga.
3. Kwamba marehemu alikuwa anamiliki kiwanja namba 7 kitalu "T" kilichopo Martin shamba katika Jiji la Tanga.
4. Kwamba katika kukusanya mali za marehemu nimetafuta hati ya kiwanja namba 7 kitalu "T" nimekosa na kwenda kutoa taarifa polisi na kupewa RB No. **TAN/TAN/RB/236161/2020 ERV No. 9910812029208.**
5. Kwamba kwa kiapo hiki naomba ofisi za Mipango Miji Jiji la Tanga wanipatie hati miliki ya kiwanja Na. 7 kitalu "T" Martin shamba kwa jina la marehemu **HATIBU JUMA HATIBU.**

**UTHIBITISHO**
Nathibitisha kuwa yote niliyoyatamka hapo juu ni kweli tupu na kwa kutia nguvu kiapo hiki nimefika mbele ya Hakimu Mahakamani na kuthibitisha yote hapo juu kuwa ni kweli.

115770502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**MC A/63)**
**Mahakama ya mwanzo ya ............ Arusha Mjini**
**Wilaya ya ..................................Arusha**
**MADAI NAMBARI 146 YA 2020**
**Mdai : Juliana Elirehema Raphaeli**
**amdai**
**Mdaiwa.....................smail Majid**

**Kwa: Ismail Majid wa Njiro**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za madai):-
Fika Mahakama ya bila kukosa kujibu madai ya Tsh 1,470,000/=
Kwa hiyo unahitajika /mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya tarehe 18-6-2020 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kutoa mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo.
Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshidwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 10-6-2020.

## KUPOTEA KWA CHETI



115770402

**Aliselius Alistides** anatangaza kupotea kwa chati cha kidato cha nne chenye **index namba S.0841/0116** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2017 katika shule ya Sekondari Humura. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **ILA/RB/1202/2020**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA:45..2020**
**Mdai: FATMA ABDALLAH MSOKO**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: RAMADHAN KHAMISI MFINANGA**

**Kwa:**
**RAMADHAN KHAMISI MFINANGA**

**Ombi la Mdai: FATMA ABDALLAH MSOKO**

**Madai ya: TARAKA, MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO YA MTOTO MMOJA TSH.50,000/= KWA MWEZI.**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 23 mwezi 06 mwaka 2020 saa 02:30 Asubuhi.
Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 10 mwezi 06 mwaka 2020.

115770502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;141/2020**

**Ombi la SHAMIMU ABDALLAH MATAMBO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MATAMBO IBRAHIM MATAMBO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 18/06/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/06/2020.

115770602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;135/2020**

**Ombi la MALEZYA KAPYOLO MKANTULA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MAULID ISSA MAGANGA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 06/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/06/2020.

115770902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;138/2020**

**Ombi la NEEMA MIRAJI ALLY Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu RAJABU BAKARI MUHUWILA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 03/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 04/06/2020.

115771102

## KUPOTEA KWA CHETI



115770802

**AGRIPINA K. MASAY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.2386/0001/2014** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia TLAWI SEKONDARI mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Control No. 9910810647801.**


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0782253676*


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

## Mamia wajitokeza kumzika George Floyd

**WASHINGTON, Marekani**

MAMIA ya waombolezaji walijaa kwenye Kanisa la Fountains of Praise, Houston, Texas juzi kumuaga, Floyd ambaye kifo chake kilitokana na kukamatwa na polisi.

Tangu kutokea kwa kifo cha Floyd, maandamano nchini Marekani yalishika kasi dhidi ya ukatili wa polisi na ubaguzi wa rangi.

Wanasiasa, wanaharakati wa haki za kiraia na wasanii waliungana na familia kutoa sifa za mtu aliyejulikana kama 'Jitu Mpole' kabla ya jeneza lake la rangi ya dhahabu kusafirishwa kwa kuvutwa na farasi weupe hadi kaburini kando ya kaburi la mamake.

"Tunaweza kulia, tunaweza kuomboleza, tutapata faraja na tutakua na matumaini" alisema kasisi mwenza wa kanisa hilo, Mia Wright.

Floyd aliuawa Mei 25, mwaka huu na ofisa wa Polisi mzungu aliyemuwekea goti kwenye shingo yake kwa karibu dakika tisa akiwa analia na kusema "siwezi kupumua, siwezi kupumua", maneno yaliyogeuka kuwa kero cha kuwaleta pamoja waandamanaji.

Kifo chake kimeleta mwangaza juu ya mvutano wa jadi kati ya jamii ya watu weusi na polisi nchini Marekani, na kwengineko duniani pale maelfu na maelfu ya watu walijitokeza kuandamana katika miji mikuu tofauti kulaani kitendo hicho na kupinga ubaguzi wa rangi.

**VOA**

## Ripoti: Visa vya ubaguzi vimeongezeka Ujerumani

**BERLIN, Ujerumani**

RIPOTI ya kila mwaka ya Shirika la Kupambana na Ubaguzi wa rangi nchini Ujerumani (ADS) limesema ubaguzi wa watu kwa misingi ya asili yao umeongezeka nchini humo, na kuonya juu ya madhara makubwa kwa jamii.

Kwa mujibu wa ripoti ya kila mwaka ya 2019 iliyowasilishwa juzi na shirikisha hilo, idadi ya visa vya ubaguzi wa rangi vilivyoripotiwa nchini humo iliongezeka kwa asilimia 10 hadi 1,176.

Ilieleza kuwa visa hivyo vinachangia asilimia hadi 33 ya visa vinavyoshughulikiwa na wakala huo.

Ilieleza kuwa mwaka 2016, ilikuwa asilimia 25, mwaka 2015 vilikuwa visa 545 viliporipotiwa, lakini kwa sasa idadi imeongezeka zaidi ya mara mbili

Tangu kifo cha mmarekani mweusi, George Floyd kilichorekodiwa kwenye video, maandamano yamefanyika sehemu mbalimbali duniani ikiwamo Ujerumani.

Watu wengi nchini Ujerumani walishtushwa na video ya kifo cha maumivu alichopitia Floyd baada ya kuwekewa goti na kukandamizwa shingoni kwa takribani dakika tisa na askari polisi mweupe.

Maelfu ya watu waliingia mitaani nchini Ujerumani kupinga mauaji hayo licha ya vizuwizi vilivyowekwa kudhibiti mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Katika wakati ambapo kuna nadhari kubwa ya vyombo vya habari, waandamanaji hao wamelalamika juu ya ubaguzi wa rangi nchini Ujerumani.

DW

# Serikali: Nkurunziza hakufa kwa corona

**BUJUMBURA, Burundi**

SERIKALI ya Burundi imeeleza rasmi kwamba kifo cha Rais Pierre Nkurunziza, kilisababishwa na ugonjwa wa moyo.

Msemaji wa serikali ya Burundi alisema kuwa Rais Nkurunzinza alifariki kutokana na maradhi ya moyo na kwamba alipelekwa hospitali ya jimbo la Karuzi mwishoni mwa wiki liyopita.

"Kwanza alipata afueni, lakini ilipofika Jumatatu hali yake iligeuka na kuzidi kuwa mbaya. Nkurunziza alikufa akiwa na umri wa miaka 55. Mke wake alipelekwa Kenya jumatatu hiyo hiyo kwa ajili ya matibabu ya corona," alisema msemaji wa serikali ya Burundi.

Nkurunziza amekufa wakati Rais mteule, Evariste Ndayishimiye anatarajiwa kuapishwa rasmi kushika madaraka wiki chache zijazo. Ndayishimiye alishinda uchaguzi wa rais nchini Burundi mwezi uliopita, baada ya Nkurunziza kuamua kutogombea muhula mwingine.

Kifo chake ni kama tetemeko la ardhi nchini Burundi baada ya kuitawala nchi hiyo kwa muda wa miaka 15.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanasema sasa Burundi haiwezi tena kuficha ukweli juu ya janga la corona baada ya kifo cha kiongozi huyo na baada ya mke wake kupelekwa Nairobi kwa ajili ya matibabu ya maradhi hayo.

Hapo awali wachambuzi walitarajia kumwona Nkurunziza akivuta hatamu za uongozi nyuma ya kiongozi mpya Ndayishimiye.

Mtaalamu wa masuala ya kisiasa, Thierry Vircoulon alisema huenda kifo cha Nkurunziza kimetokana na mkakati wa kisiasa.

Wiki moja ya maombolezo

Wakati huohuo, Serikali ya Burundi imetangaza wiki moja ya maombolezo kutokana na kifo cha rais Nkurunzinza.

Kutokana na kifo cha Rais Nkurunzinza, viongozi wa mataifa mbalimbali wametoa salaam zao za rambirambi.

Rais wa Tanzania, John Magufuli, Rais wa Rwanda, Paul Kagame , Macky Sall wa Senegal ni miongoni mwa marais waliotoa salamu hizo.

Kwa mujibu wa katiba ya Burundi, Rais anapofariki akiwa madarakani kabla hajakabidhi madaraka kwa rais mwingine, Spika wa Bunge anachukua madaraka na kutayarisha uchaguzi mwingine.

***DW***



Wananchi wakiwa wamekusanyika pembezoni mwa barabara kuuaga mwili wa George Floyd ambao ulikuwa umebebwa kwenye gari la farasi. **PICHA: AFP**

# EU wafika Goma kupambana na ugonjwa corona, ebola

**KINSHASA, Congo**

UJUMBE wa ngazi ya juu wa Umoja wa Ulaya (EU) umewasili katika mji wa Goma mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), kuunga mkono juhudi za kupambana na maradhi ya ugonjwa wa corona na ebola.

Ujumbe huo pia unalenga kuhimiza upatikanaji wa suluhisho katika mizozo inayolikumba eneo hilo.

Kabla ya kusafiri kwenda Goma, ujumbe huo ulifanya mazungumzo na Rais wa nchi hiyo, Felix Tshisekedi mjini Kinshasa.

Ujumbe huo unawajumuisha, Kamishna wa EU anayehusika na usuluhishi wa mizozo, Janez Lenarcic, pamoja na waziri wa Mambo ya Nje wa Ufaransa, Jean Yves Ledrian ambaye ni kiongozi wa ujumbe huo.

Akizungumza mjini Goma, Ledrian alisema kwamba watawasaidia wakazi wanaoendelea kukabiliana na janga la virusi vya corona nchini humo.

Baada ya kuwasili kwa ujumbe huo, wawakilishi wengine wa EU waliwasili mjini Goma wakiwa na vifaa vinavyokuwa na uwezo wa kusaidia kupungua maambukizo ya virusi vya corona na ebola ndani ya maeneo yanayo athirika na majanga hayo.

Wakati huohuo, Gavana wa mkoa huu wa Kivu ya kaskazini, Carly Nzanzu Kasivita, akizungumza na vyombo vya habari alithibitisha kuwa EU umeahidi kuitolea serikali ya Congo dola milioni 40 za marekani, katika lengo lakusaidia kudhibiti kusambaa kwa ugonjwa wa Corona.

Kwa upande wao wakazi mjini Goma wameonyesha hisia zao kwa kutoa maoni kuhusu msaada huo ulioletwa na wajumbe wa EU.

Kutolewa kwa msaada huo kumefuatia wakazi waishio mji wa Kivu ya Kaskazini kuendelea kukabiliana na ugonjwa wa ebola, huku idadi ya vifo ikiwa ni zaidi ya 2,000 na wengine 53 walithibitishwa kuambukizwa virusi vya corona tangu kutangazwa nchini humo.

***DW***




# MESSI
## FITI KUIVAA MALLORCA, ASEMA SETIEN

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Quique Setien amesema hakuwa na "shaka yoyote" juu ya 'ufiti' wa Lionel Messi, wakati nahodha huyo akijiandaa kuivaa Real Mallorca.

Messi alirudi kwenye mazoezi ya makundi Jumatatu baada ya kupata maumivu na hivyo alilazimika mshindi huyo mara sita wa tuzo ya Ballon d'Or kujifua peke yake.

Msimu wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, unarudi Alhamisi baada ya kusimama kwa miezi mitatu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, huku vinara Barca - ambao wanaongoza kwa pointi mbili kileleni wakicheza dhidi ya Real Madrid, huku mechi 27 zikiwa zimeshachezwa watakwenda nyumbani kwa Mallorca Jumamosi.

Messi anatarajia kuivaa Mallorca baada ya Setien kuiambia redio Catalunya: "Hatukuwa na shaka yoyote juu ya uwezo wake dhidi ya Mallorca.

"Pia kumekuwa na majeruhi wengine. Hivyo nina uhakika tutakuwa naye kwenye kikosi chetu."

Wakati huo huo, Luis Suarez amebainishwa kwamba yupo fiti kuichezea Barca katika mechi zao 11 zilizobaki kumaliza msimu wa 2019/20 baada ya kupona kutokana na operesheni ya goti aliyofanyiwa Januari.

Suarez alifanyiwa upasuaji wa goti la kulia mwanzoni mwa mwaka huu, huku akiripotiwa kutokuwa kwenye kiwango chake kwa miezi kadhaa.

Hata hivyo, Setien, hana uhakika kama fowadi huyo wa kimataifa wa Uruguay mwenye umri wa miaka 33 kama ataanza kwenye mchezo huo wa ugenini dhidi ya Mallorca.

"Ni kitu fulani tunachoweza kuzungumza," alisema Setien.

"Sina uhakika kama ataweza kucheza kuanzia mwanzo. Litakuwa sio jambo zuri kwake yeye kucheza kwa mechi yote."

## NYOTA WATATU 'WAMUUMIZA' KICHWA KLOPP

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp bado hajajua hali ya nyota wake watatu muhimu kwenye kikosi cha kwanza cha Liverpool, wakati huu wakijiandaa kurejea kwa Ligi Kuu England.

Kwa mujibu wa ripoti zinadai mabingwa hao watarajiwa wa Ligi Kuu England msimu huu wamekuwa kwenye mashaka makubwa juu ya hali ya kiafya ya wakali hao watatu ambao ni Mohamed Salah, Andrew Robertson na Georginio Wijnaldum katika kuelekea kuanza kwa mechi za soka ili kumalizika msimu.

Liverpool wataanza kwa kukabiliana na wapinzani wao wa jiji moja, Everton mchezo utakaopigwa Juni 21 mwaka huu, huku kikosi hicho cha Klopp kikihitaji walau mshindi mmoja tu kuhitimisha ndoto zao za kunyakua taji hilo ambalo wamesotea kulipata kwa miaka 30.

Hata hivyo, wababe hao wa Anfield wanaweza kukosa huduma ya mastaa wake hao watatu katika mechi ya kwanza na ripoti zinadai Salah, Robertson na Wijnaldum wote walionekana kuwa nje kwenye mezoezi ya siku za karibuni.

# Herrera: Najivunia kumkaba Hazard

**PARIS, Ufaransa**

ANDER Herrera ametaja tukio la kumdhibiti aliyekuwa kiungo wa Chelsea, Eden Hazard katika mchezo wa Ligi Kuu England uliochezwa Aprili mwaka 2017 wakati akichezea Manchester United kuwa la kipekee kwake.

Katika mchezo huo ambao United waliibuka na ushindi wa mabao 2-0 nyumbani, Herrera alifanikiwa kumfanya Hazard aliyekuwa tishio kipindi hicho asifurukute na kuiwezesha timu yake kuibuka na ushindi huo muhimu.

Herrera ambaye kwa sasa anaitumikia PSG, amedai alifurahishwa na jinsi alivyoweza kuyamudu majukumu mapya aliyopewa na kocha Jose Mourinho kwa ajili ya kumdhibiti Hazard katika mechi hiyo.

"Jose alijua kuwa Hazard ni mmoja kati ya wachezaji bora, na ili tufanikiwe kushinda tulihitaji kumfanya asiguse mpira," amesema Herera katika mahojiano ya kupitia Instagram live. "Nilimwambia Jose kuwa nipo tayari kama angenihitaji, na nilimfuata kila mahali, hata kama angeenda bafuni ningemfata kwani nilihitaji kushinda mechi ile."

Herera alibainisha kwamba, hilo lilikuwa jambo muhimu sana katika maisha yake ya mpira na alikuwa na furaha kubwa baada ya mchezo huo.

Hata hivyo, amemtaja Hazard kama mmoja wa viungo bora kabisa duniani kwa sasa na ana imani akiwa kule Real Madrid atarudi kwenye kiwango chake baada ya kukumbwa na majeruhi.

## HABARI MICHEZO




# ARSENAL
## YAJIPANGA KUUZA NYOTA WAKE

**LONDON, England**

MIKEL Arteta anapanga kuwauza nyota wengi wa kikosi cha Arsenal wakati wa dirisha la majira haya ya joto litakapofunguliwa, ili kupata fedha za usajili wachezaji wapya, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Wachezaji nyota kama, Pierre-Emerick Aubameyang, Alexandre Lacazette na Mesut Ozil ni miongoni mwa wachezaji wanaotajwa watafunguliwa mlango wa kutokea.

Ripoti hiyo imesema, Arteta amepanga kuwaondoa mabeki wake wanne ili kufungua njia kwa wengine kujiunga na timu hiyo.

Mabeki wanaotajwa kuwa kwenye uwezekano wa kuuzwa ni pamoja na Shkodran Mustafi, Sokratis Papastathopoulos, Rob Holding na Sead Kolasinac.

Aidha, ripoti hiyo inasema Arteta anataka kumbakiza David Luiz - ambaye ameripotiwa kuongezwa mkataba mpya.

Kwenye dirisha linalokuja na majira ya joto Arsenal itamkaribisha kikosi beki William Saliba, ambaye walimsajili kutoka Saint-Etienne kwa pauni milioni 27.

Hivyo Saliba na Luiz watakuwa nguzo mpya kwenye safu ya mabeki, wakati kocha Arteta atakapopitisha fagio kuondoa wale anaodhani wanapaswa kuondoka ili kutengeneza kikosi kipya kitakachokuwa na vijana wengi.

# Madrid yawekewa ngumu kwa Odegaard

**MADRID, Hispania**

MARTIN Odegaard ataendelea kubakia Real Sociedad kwa msimu mwingine, Rais wa Jokin Aperribay, amesema.

Odegaard amekuwa na msimu mzuri katika klabu hiyo yenye mkataba naye wa mkopo wa muda mrefu akitokea Real Madrid, amefunga mabao saba na kutoa pasi za mwisho nane kwenye michezo 28 aliyocheza ya mashindano mbalimbali.

Na klabu hiyo ina ruhusa ya kumwongezea mkopo na kubakia klabuni hapo kwa mwaka mmoja zaidi.

"Nafikiri Odegaard ataendelea kubakia Real. Ndio kitu ninachokiamini na ndio matumaini yangu,"



Aperribay alikiambia kituo cha Radio Euskadi.

"Kama unakaa Real, unatakiwa utuhakikishie uwezo huo, kama alivyokuwa mwaka jana. Ushawishi ndio uamuzi sahihi kwa ajili ya msimu ujao.

"Uamuzi umebakia kwake mwenyewe na ninafikiri atabakia hapa."

Klabu mbalimbali za barani Ulaya ziliwania saini ya nyota huyo raia wa Norway kabla Madrid haijashinda vita hiyo kwa kumsajili mwaka 2015 wakati Odegaard akiwa na umri wa miaka 16.

Tangu alipotua Bernabeu, ameshindwa kupata namba katika kikosi cha kwanza cha Madrid, akiwa amecheza mechi mbili tu za timu ya wakubwa na mabosi wake waliamua kumtoa kwa mkopo kwenye klabu tatu tofauti.

Odegaard, ambaye anahusishwa kutakiwa na AC Milan, ameonyesha kiwango kizuri akiwa na Heerenveen, Vitesse Arnhem na Sociedad.

# Newcastle bado wamtaka Coutinho

**LONDON, England**

NEWCASTLE tayari imeshaanza mazungumzo rasmi ya kumsajili kiungo wa Barcelona, Philippe Coutinho, taarifa mbalimbali zimeripoti.

Kiungo huyo wa zamani wa Liverpool kwa sasa yuko kwa mkopo kwa vigogo wa Bundesliga, Bayern Munich lakini hawatamsajili moja kwa moja ifikapo mwisho wa msimu.

Coutinho amekosa namba katika kikosi cha Katalunya baada ya kushindwa kung'ara kwenye timu hiyo kama walivyotarajia licha ya kutumia kiasi kikubwa cha fedha walipomsajili akitokea Anfield, Januari, mwaka 2018.

Tottenham pia imeonyesha nia ya kumsajili kiungo huyo mchezeshaji wa Timu ya Taifa ya Brazil na majira ya joto mwaka jana walikaribia kukamilisha mchakato huo kabla ya kuamua kwenda Alliaz Arena.

Kocha Carlo Ancelotti anavutiwa na mchezaji huyo na anaonekana anajiandaa kumrejesha Coutinho ndani ya Merseyside, wakati Arsenal, Manchester United na Chelsea wanaonekana wanajipanga pia kumsajili kwa mkopo.

Lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 anaonekana chaguo lake ni kutua Tyneside, endapo Waarabu wa Saudi Arabia ambao wameweka dau la pauni milioni 300 watafanikiwa kuimiliki klabu hiyo, linaandika France Football.

Uamuzi wa kuwapa Waarabu hao timu kutoka kwa Mike Ashley, utatolewa baada ya kukamilika kwa uchunguzi ambao pia unazihusisha klabu kubwa za England.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR AENDELEA KUIOTA BARCELONA

Hata hivyo kutikisika kwa uchumi kulikosababishwa na janga la corona, kunaweza kuifanya...

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR ameripotiwa kuwa bado hajakata tamaa juu ya mpango wake wa kurejea kuichezea Barcelona, kwa mujibu wa gazeti la Mundo Deportivo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil anaamini mchakato wake wa kurejea kwa vigogo hao wa Hispania unaweza kukamilishwa katika kipindi hiki cha majira ya joto.

Nyota huyo wa Paris Saint-Germain, aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya pauni milioni 198 wakati akitokea, Barcelona amekuwa akihusishwa na mpango wa kurejea pale Nou Camp.

Wakati wa dirisha la usajili la majira ya joto lililopita, Neymar aliripotiwa angerudi Nou Camp, lakini miamba hiyo ya LaLiga ilishindwa kuafikiana na mabingwa wa Ligue 1 na hivyo mkali huyo akaendelea kubaki jijini Paris msimu huu.

Wakati hivi sasa Barcelona wakiwa wameripotiwa kuiwania saini ya straika wa Inter Milan, Lautaro Martinez, janga la corona linaonekana kusababisha madhara makubwa kiuchumi na hivyo linaweza kuharibu mpango wao wa kumrudisha Neymar.

Hata hivyo, Mundo Deportivo limeandika, Neymar mwenye umri wa miaka 28, hajakata tamaa juu ya kurejea kujiunga na Barcelona kwa ajili ya msimu wa 2020/21.

Neymar ameendelea kuonyesha kiwango bora huko PSG licha ya kusumbuliwa na majeruhi mara kadhaa, ambapo kwa msimu huu amefunga mabao 18, na kutoa pasi za mwisho 10 katika mechi 22 alizocheza kwenye mashindano yote.

Barcelona pia itatakiwa kulipa ada ya pauni milioni 99 ambayo imetajwa katika mkataba ili kunasa saini ya straika wa Inter Milan, Lautaro Martinez kabla ya Julai 7, mwaka huu, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Inter Milan, CEO Beppe Marotta aliliambia gazeti hilo la Hispania.

"Ngoja tuone kwanza Barcelona watakachokifanya halafu tutakaa mezani na mchezaji kuangalia nini kitafuata."

Martinez amebakiza miaka mitatu katika mkataba wake na klabu hiyo ya San Siro, akiwa amefunga magoli 16 na kutoa pasi za mwisho nne kwenye michezo 31 aliyocheza kabla ya ligi na mashindano mbalimbali kusimamishwa kutokana na corona.

## KWA UFUPI

**CHELSEA YAMGEUKIA KAI**

CHELSEA inaamini mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (20), atajiunga na Manchester United, hivyo wamehamishia nguvu zao kuwania saini ya kiungo mshambuliaji wa Bayer Leverkusen Mjerumani, Kai Havertz. ***(ESPN)***

**BENRAHMA ANUKIA CHELSEA**

MABOSI wa Chelsea wamemweka kwenye orodha ya wachezaji inaowahitaji katika kipindi cha majira ya joto, winga wa Brentford, Said Benrahma. Astona Villa pia inatajwa kumhitaji nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Algeria. ***(Guardian)***

**MARTINEZ KUIKAMUA BARCA**

HADI kufikia Julai 7, mwaka huu, vigogo wa Hispania watatakiwa kulipa ada ya pauni milioni 98 ili kumnasa straika wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Argentina, Lautaro Martinez, kama ilivyotajwa kwenye mkataba wake. ***(Sky Sports)***

**SILVA ATOA MSIMAMO**

BEKI wa kati wa Timu ya Taifa ya Brazil, Thiago Silva, amesema bado anataka kubakia Ulaya baada ya kuelezwa na Paris St-Germain kwamba mkataba wake hautaongezwa, na anaamini ana nafasi ya kusajiliwa na klabu nyingine kubwa kwa misimu miwili. ***(ESPN)***

**TIMU 5 EPL ZACHUANA**

KLABU tano za England ambazo ni pamoja na Arsenal, Everton, Newcastle, West Ham na Wolves, zimeweka wazi nia yao ya kumsajili golikipa mkongwe wa PSG ambaye ana umri wa miaka 35. ***(90 Minutes)***

**AUBA, ARSENAL KITAELEWEKA**

ARSENAL inaamini uhusiano wake mzuri na wakala wa straika Pierre-Emerick Aubameyang (30), ambaye ni baba yake, utawasaidia kukamilisha mazungumzo ya nyota huyo kukubali kusaini mkataba mpya wa kubakia The Gunners. ***(Telegraph)***

**TAGLIAFICO AGOMBEWA**

LEICESTER City imemtaja beki wa kushoto wa Ajax na Timu ya Taifa ya Argentina, Nicolas Tagliafico (27), kuwa anafaa kurithi nafasi ya Ben Chilwell, ambaye anawindwa na Chelsea na Manchester City. ***(Mirror)***

**UNITED YAMHITAJI JAMES**

MANCHESTER United imesema haitakuwa tayari kumruhusu winga wa Timu ya Taifa ya Wales, Daniel James (22), kuondoka klabuni hapo kwa mkopo kama haitafanikiwa kunasa saini ya mshambuliaji wa England, Jadon Sancho. ***(Manchester Evening News)***

**RB KUMUUZA UPAMECANO**

RB Leipzig imeweka wazi iko tayari kumuuza beki wake Mfaransa Dayot Upamecano (21), ambaye anawindwa na Arsenal, kuliko kumwacha aondoke akiwa mchezaji huru baada ya mkataba wake kumalizika ifikapo Juni, mwakani. ***(Bild)***

**GUEYE KUONDOKA PSG**

KIUNGO wa Paris St-Germain, Idrissa Gueye, amesema hana nia ya kuondoka ingawa mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa wameweka wazi Msenegal huyo anaweza kurejea katika Ligi Kuu England. Wolves na klabu yake ya zamani ya Everton zimeonyesha nia ya kuhitaji huduma yake. ***(Le10Sport)***

**SPURS, EVERTON VITANI**

SOUTHAMPTON inaonekana kukataa kupokea ada chini ya pauni milioni 35 ili kumuuza nyota wake, Pierre-Emile Hojbjerg. Kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Denmark ambaye ana umri wa miaka 24 anawindwa na Everton pamoja na Tottenham. ***(Evening Standard)***

HABARI MICHEZO

# AZAM BADO YAWAOTA 'MAPRO' WALIOKWAMA

Na Saada Akida

HUKU zikiwa zimesalia siku tatu ili kurejea kwa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Azam FC, Aristica Cioaba, amesema kukosekana kwa nyota wake saba wa kimataifa kumeathiri mipango yake na hali hiyo inamweka kwenye wakati mgumu.

Cioaba ameliambia gazeti hili wachezaji hao wanaocheza katika nafasi muhimu kwenye kikosi cha kwanza bado wamekwama kwenye nchi zao kutokana na 'Lockdown' iliyosababishwa na janga la corona.

Kocha huyo aliwataja wachezaji hao ni mabeki wawili, Yakubu Mohammed, Daniel Amoah, golikipa chaguo la kwanza, Razack Abarola (Ghana), Bruce Kangwa, Never Tigere na Donald Ngoma (Zimbabwe) na Nicholas Wadada ambaye ni Mganda.

Alisema amekuwa na pengo kubwa katika kikosi chake ambalo limeathiri mipango yake na ana wasiwasi wa kufikia malengo waliyokuwa nayo kwenye msimu huu.

"Kuwakosa nyota hao inaniumiza kichwa, kwa sababu sina uhakika kama watakuwa sehemu katika mipango ya kikosi katika michezo ya kwanza ya ligi, hii inaniumiza sana," alisema Cioaba.

Aliongeza kukosekana kwa nyota hao kumnamlazimika kuwapandisha wachezaji kutoka katika timu ya vijana ambao wanahitaji zaidi ya wiki mbili ili kuingia katika mfumo wake.

"Ni vigumu wachezaji hao wa kimataifa kuwahi michezo ya mwanzo, sasa natumia muda huu kuhakikisha kuwajenga wachezaji kutoka katika kikosi cha vijana, ili kuwa mbadala wa nyota wa kimataifa," alisema kocha huyo.

Kikosi hicho kinachofanya mazoezi mara mbili kwa siku ili kuhakikisha wachezaji wote wanakuwa imara na tayari kutengeneza 'kombinesheni' itakayosaidia kuvuna matokeo mazuri kwenye mechi zote watakazocheza zilizobakia.




Mafundi wakiendelea na ukarabati kwenye Uwanja wa Azam Complex, ulioko Chamazi jijini, Dar es Salaam tayari kwa michezo ya Ligi Kuu Bara itakayorejea tena kuanzia Jumamosi. **PICHA: AZAM**

# JKT Tanzania yaipania Yanga

Na Shufaa Lyimo

WATATUJUA! Hayo ni maneno ya uongozi wa JKT Tanzania kuelekea mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga itakayochezwa Juni 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma.

Ofisa Habari wa JKT Tanzania, Jamila Mutabazi, aliliambia gazeti hili kikosi chake kinaendelea vema na mazoezi na wachezaji wote wako tayari na mchezo huo ambao utakuwa ni wa kwanza kwao tangu kurejea kwa Ligi Kuu. "Kikosi chetu kinaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kukutana na mahasimu wetu, tunajua haitakuwa mechi rahisi, ila tumejipanga kwa ajili ya kusaka ushindi tu," alisema Mutabazi.

Aliongeza JKT Tanzania imejipanga kurejea 'kivingine' katika ligi hiyo baada ya wachezaji kurejea tena uwanjani kusaka pointi muhimu kwenye kila mchezo.

"Tutarudi na kasi kubwa ili tuweze kumalizia msimu huu wa ligi kwa kuhakikisha tunamaliza katika nafasi za juu katika msimamo, hayo ndio malengo yetu," Mutabazi alisema.

Aliongeza wachezaji wake walitumia vema kipindi cha mapumziko kwa kufanya mazoezi kikamilifu kama walivyotakiwa na makocha wao na hakuna mchezaji aliyekutwa ameshuka kiwango.

Katika msimamo wa ligi, JKT Tanzania iko katika nafasi ya saba ikiwa na pointi 42, baada ya kushuka dimbani mara 28.

## Ndanda yasaka pointi 12 Bara

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Ndanda FC ya Mtwara, Meja mstaafu Abdul Mingange amesema anahitaji kupata pointi 12 katika mechi zake tisa zilizosalia ili timu hiyo ibakie kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mingange alisema mbali na changamoto ya ukata wa kifedha waliokuwa nayo, kikosi chake hakijakata tamaa na kimejipanga kuendelea kupambana ili kutimiza malengo yao.

Mingange alisema ni ngumu kwa mchezaji asiyelipwa posho na malimbikizo ya mishahara kufanya vizuri, lakini nyota wake wameahidi kupambana hadi dakika ya mwisho ya msimu huu.

Kocha huyo alisema kikosi chake kina wachezaji majeruhi wawili ambao ni pamoja na Samuel John na Godfrey Malibicha, na nyota hao hatawatumia katika michezo yao ya kwanza ya ligi hiyo.

"Kwa hali yote hiyo, lakini bado tunapambana kuhakikisha tunashinda michezo yetu yote na kupata pointi 12 ili kujinusuru katika nafasi ya kushuka daraja, tukifikisha pointi 42, tutakuwa tumenusurika," alisema Mingange.

Alisema anafahamu michezo yote iliyobakia itakuwa na ushindani kwa sababu kila timu itahitaji kurekebisha makosa yake ya mechi zilizotangulia.

"Tupo ICU, ila ninawahakikishia wadau wa soka hatutashuka daraja, licha ya kuwapo kwa changamoto ya ukata wa kifedha pamoja na majeruhi," Mingange aliongeza.

## Wachezaji Polisi Tanzania kuuzwa

Na Shufaa Lyimo

BENCHI la Ufundi la Polisi Tanzania limesema liko tayari kuruhusu wachezaji wanaotaka kuondoka katika timu hiyo na kwenda kwenye klabu nyingine kutafuta maisha.

Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, aliliambia gazeti hili anajisikia faraja kuona mchezaji wake anahitajika na klabu nyingine, kwa sababu malengo ya kupandisha vipaji yatakuwa yamefanikiwa.

Malale ambaye timu yake inatumia Uwanja wa Chuo cha Polisi Moshi, mkoani Kilimanjaro alisema mchezaji anaona 'faida' kwa mchezaji wake kuhamia mahali kwingine.

"Ninafurahi kusikia mchezaji wangu anapata nafasi sehemu nyingine, kwa sababu najua anapata mafanikio na maendeleo, ilimradi taratibu za uhamisho zifuatwe," alisema Malale.

Kocha huyo alisema pia atafurahi zaidi kuona mchezaji anakwenda kujiunga na klabu kubwa za hapa nchini na anajua atapata nafasi zaidi ya kutangaza kipaji chake na hivyo atatimiza malengo yake.

Alisema kikosi chake kinaendelea vizuri na mazoezi na anaamini watafanya vema katika mechi zote za Ligi Kuu Bara zilizobakia.

Michezo
Alhamisi Juni 11, 2020
Nipashe



## Neymar aendelea kuiota Barcelona

HABARI UK 22

# YANGA, MOLINGA KIMENUKA

●●●Akacha safari ya Shinyanga na kudai anaonewa, Mkwasa akanusha na kuahidi hatua kali...

**Faustine Feliciane na Shufaa Lyimo**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael akirejea nchini, wachezaji Papy Tshishimbi na David Molinga wameachwa katika kikosi kilichoelekea Shinyanga kuwakabili wenyeji Mwadui FC kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa keshokutwa mkoani humo.

Hata hivyo, Tshishimbi ameachwa katika safari hiyo kutokana na kuwa majeruhi, wakati Molinga ameibuka na kueleza ameshindwa kuambatana na kikosi hicho kwa sababu hakuwa kwenye mipango ya Kocha Msaidizi, Bonifcae Mkwasa.

Taarifa za awali zilidai Molinga amegomea kusafiri na timu kwenda Shinyanga bila kutoa sababu na alikuwa kwenye orodha ya nyota 22 waliotajwa na Mkwasa.

Molinga aliliambia gazeti hili baada ya kufahamu hayuko kwenye orodha ya wachezaji wanaosafiri, aliamua kwenda kulala nyumbani kwake na si kambini ambapo nyota wengine wa timu hiyo walilala kwa ajili ya kujiandaa na safari hiyo.

"Sio kweli kuwa nimegomea kusafiri, natupiwa lawama na mabaya yote mimi, sikuwapo katika majina yaliyotajwa na kocha kusafiri na ndio maana nilirudi nyumbani nikiwaacha wale wanaosafiri kambini, ili kesho yake waanze safari," alisema Molinga na kuongeza.

"Nimeshangaa nikaja kushtukizwa nyumbani muda mfupi kabla ya safari, mimi nimetoka kwetu kuja kufanya kazi hapa, na kazi yangu ni mpira sasa kwa nini nigomee safari?, kuna vitu viongozi wanaficha," Molinga alisema.

Mshambuliaji huyo alisema amekuwa akifanya mazoezi na timu na hakuwahi kukosa lakini hakutajwa kwenye kikosi cha wachezaji wanaosafiri na alikubaliana na uamuzi huo na kuamua kurejea nyumbani kwake.

"Baadaye nakuja kushtukizwa nisafiri, najua labda sitakiwi kwenye timu na mkataba wangu unamalizika na ninaondoka," alisema Molinga.

Mkurugenzi wa Mashindano ya Yanga, Thabit Kandoro, alisema mshambuliaji huyo amekuwa mtovu wa nidhamu na hii si mara ya kwanza kugomea safari.

Kandoro alisema Molinga aliwahi kugoma kusafiri na timu wakati wanakwenda kuikabili Namungo na Polisi Tanzania na alipoulizwa kwa nini amefanya hivyo, alitupia lawama kwa viongozi ambao hawakuwa na kosa lolote.

"Mimi ndio naandaa taratibu zote za safari ya timu, pamoja na kuandaa malipo yao na kuyawasilisha katika ofisi ya uhasibu, nilipewa orodha ya wachezaji wanaosafiri siku nne kabla na jina la Molinga lilikuwapo, sasa anasemaje hayumo kwenye safari?" alihoji Kandoro.

Alisema wamesikia utetezi wake na uongozi utakutana na kuifanyia kazi kauli aliyoisema kama walivyofanya wakati alipofanya makosa mengine siku za nyuma. Naye Mkwasa alisema amekerwa na kitendo alichokifanya mshambuliaji huyo na anashangaa kusikia Molinga anasema jina lake halikutajwa kwa ajili ya kujiandaa na safari hiyo.

"Jina la Molinga lilikuwapo kwenye orodha yangu ya leo (jana), wenzake walisikia nilipokuwa naita kila mmoja alikuwa anaingia chumbani na wengine walikuja baadaye, leo (jana) asubuhi tulimpigia simu saa 10: 00 asubuhi, tumemsubiri sana hajatokea, tukiwa ndani ya basi hakutokea, ikabidi tuondoke," alisema Mkwasa. Kocha huyo alisema hii ni mara ya tatu kwa Mkongomani huyo kugoma kusafiri na timu na ameahidi hilo watalifanyia uamuzi haraka.

"Leo ni mara ya tatu Molinga kugoma kujiunga na timu, naona amefanya mazoea sasa lazima tumchukulie hatua," Mkwasa alisisitiza.

Aliongeza Kocha Mkuu Eymael ataungana na kikosi hicho baada ya jana kurejea nchini akitokea kwao Ubelgiji.

Nyota 19 wa kikosi cha Yanga waliondoka jijini jana kuifuata Mwadui na baada ya mechi hiyo, watasafiri kuelekea Dodoma kucheza dhidi ya wenyeji JKT Tanzania.



Mshambuliaji wa Yanga, Mkongomani David Molinga, ambaye anatarajiwa kuukosa mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Mwadui FC utakaochezwa Jumamosi baada ya kuachwa jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# Simba yaanza kuhesabu dakika

**Na Somoe Ng'itu**

LICHA ya janga la Corona kuchelewesha msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara kumalizika mapema, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, amesema wana nafasi ya kutetea ubingwa wa ligi hiyo mapema zaidi.

Mabingwa hao watetezi wanaongoza katika msimamo wa ligi wakiwa na pointi 71 na wanahitaji pointi 15 tu katika michezo 10 iliyosalia ili kulichukua kombe hilo kwa mara ya tatu mfululizo.

Akizungumza na gazeti hili, Matola alisema tofauti kubwa waliyonayo na timu zinazowakimbiza, ndio sababu inayowapa nguvu ya kuamini wana kazi nyepesi ya kukamilisha malengo yao.

**"Mlima uliobakia ni mdogo sana, kwa sababu wengine tayari wanaelekeza nguvu zaidi kwenye Kombe la FA, kama wapinzani wetu watateleza kidogo, kwetu itakuwa faraja zaidi na safari itazidi kuwa fupi, sisi mataji yote tunayajitaji na tutacheza kwa kasi ile ile," alisema nahodha huyo wa zamani wa Wekundu wa Msimbazi.**

Aliongeza kila mchezaji wa Simba amedhamiria kumaliza msimu kwa furaha na kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa mara nyingine.

Simba itaendelea na kampeni ya kuwania ubingwa Jumapili kwa kuwakaribisha Ruvu Shooting na Juni, mwaka huu itacheza dhidi ya Mwadui FC kwenye Uwanja wa Taifa na baada ya hapo itasafiri kuelekea jijini Mbeya kuwafuata Tanzania Prisons na Mbeya City.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >